Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Pili – Tarehe 30 Januari, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 14

**Hitaji la Kumuenzi Hayati Edward M. Sokoine**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa tatu Tanzania – Hayati Edward Moringe Sokoine, alifariki baada ya kupata ajali tarehe 12/4/1984 wakati akitoka Dodoma baada ya kuahirishwa kwa Mkutano wa Bunge; na kwa kuwa ili kutunza historia yetu tunahitaji kuweka alama ya kumbukumbu sehemu aliyopatia ajali:-

(a) Je, ni mamlaka gani ya Serikali yenye jukumu la kuweka alama mahali alipofia kiongozi huyo?

(b) Je, ni alama gani iliyowekwa mahali hapo; na je, Serikali inaridhika na kiwango cha alama iliyowekwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, napenda kujibu maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-
Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 18 ya Mwaka 2004 ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu na Sheria Na. 1 ya mwaka 2006 inayohusu Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa haizungumzii hitaji la kuenzi maeneo ya matukio ya ajali au sababu nyingine

zinazosababaisha vifo kwa viongozi wa kitaifa. Tunapozungumzia hitaji la kuenzi na kuhifadhi maeneo kama hayo ieleweke wazi kuwa ni suala kubwa na linalohitaji zaidi fedha na hivyo linalojitokeza zaidi ni gharama za uendeshaji.

Tangu kutokea kwa ajali hiyo Dakawa, takriban miaka 24 iliyopita, eneo la ajali ya Hayati Edward Maringe Sokoine limekuwa linatunzwa na Chama Cha Mapinduzi kupitia Umoja wa Vijana wa CCM hususan wakati wa kuwasha Mwenge ambapo wao huweka kambi pahala pale. Aidha, mahali hapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Mvomero na panatambulika rasmi kwa jina la Dakawa Sokoine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imelifanyia kazi suala hilo na kuamua kwamba Uongozi wa Mkoa wa Morogoro ndio utakuwa na jukumu la kuweka alama zinazostahli mahali alipofia Hayati Edward Sokoine, ikiwa ni kuunga mkono jitihada za Chama Tawala na wananchi kwa ujumla katika kutambua jambo hili muhimu sana.

(b) Kwa hivi sasa alama zilizopo ni mnara na jukwaa pamoja na majengo machache. Serikali itafanya uchunguzi kubaini viwango mahususi vitakavyozingatiwa katika ujenzi wa minara ya kumbukumbu ya Viongozi wa Taifa ikiwa ni pamoja na sehemu hiyo kwa lengo la kutunza historia muhimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Mnara wa kumbukumbu ya Hayati Edward Moringe Sokoine uliopo pale Dakawa Sokoine, ambako sasa ni sehemu ya Makao Makuu ya Wilaya ya Mvomero, ulijengwa vizuri nasi tutazingatia ushauri wa wataalam ili kupaboresha.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la msingi limetaka kujua ni mamlaka gani inayopaswa kuweka alama yenye hadhi inayomstahiki Hayati Waziri Mkuu. La pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipata ajali wakati anatoka Dodoma katika shughuli za kiserikali, siyo shughuli za CCM. Hivyo kama Umoja wa Vijana wa CCM wasingejitokeza wakafanya hayo waliyoyafanya ina maana kwamba Serikali mpaka sasa ingekuwa imenyamaza tu kimya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyokwishasema kwenye swali la msingi kuwa suala moja halijawekwa wazi kwani Serikali inafanya kazi kwa Sheria, Taratibu na Kanuni. Nimesema mwanzo kwamba Sheria Na. 18 ya mwaka 2004 inayohusu kuwaenzi waasisi wa Taifa letu na Sheria Na. 1 ya mwaka 2006 hazikuweka bayana ni nani anayestahili kupaenzi au kupatunza pahala pale. Na nilisema mwishoni kwamba kwa sababu sasa tuko kwenye mchakato wa kupitia taratibu za kuweza kuboresha mambo yote yanayohusu kuwaenzi waasisi au viongozi wa Taifa hili basi na jambo hilo litazingatiwa wakati wa kutekeleza. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nataka kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kupenda kuongezea majibu kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mkuchika. Kwa idadi ya makofi yaliyopigwa kufuatia suala hilo, nimetafsiri kwamba Wabunge wanataka Serikali ichukue hatua.

Kwa hiyo napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumewaelewa, tutachukua hatua zinazopasa. *(Makofi)*

Na. 15

**Barabara kwa vijiji vya pembezoni - Iramba Magharibi**

**MHE. JUMA H. KILIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Nsunsu, Mingela, Tulya, Migiliango, Doromoni, Luono, Ndurumo, Tygelo na Kidaru viko pembezoni ya Jimbo au Wilaya ya Iramba na huduma yake ya barabara ni mbovu; na kwa kuwa ili uweze kufika Makao Makuu ya Wilaya ni lazima utumie barabara kama vile Ntwike hadi Tulya hadi Kiomboi au Tulya, Tyegelo, Kidaru kisha Kisiriri hadi Kiomboi ambazo ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba:-

(a) Kwa kuwa barabara hizo ni muhimu na zinahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa; je, ni lini barabara hizo zitafanyiwa matengenezo ili ziweze kupitika kwa uhakika na kuwaondolea adha wananchi wa maeneo ya Kidaru na Tulya ambao wanaishi kwa mashaka muda wote?

(b) Kwa kuzingatia unyeti wa maeneo hayo na shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa hasa biashara ya samaki katika Ziwa Kitangiri, je, Serikali haioni haja ya kuipandisha daraja barabara hiyo ikawa ya Mkoa na kuhudumiwa na *TANROADS?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara za Migilango – Kidaru (km 16.45), Migilango – Tulya (km 6.2), Ntwike – Tulya (km 24.9), Tulya – Kisisiri (km 21.25), Kisisiri – Kiomboi (km 14.4), Kiomboi – Kidaru (km 18.9) yanahitaji fedha nyingi kutokana na ukweli kwamba barabara hizo ziko kwenye milima na bonde la ufa ambako kuna mikondo mingi ya maji inayotoka milimani na miteremko mikali inayosababisha barabara kuoshwa na maji ya mvua.

Matengenezo yanayohitajika ni pamoja na kujenga madaraja, drifti na makalavati mengi, pia kupanua barabara kwa kuchonga miamba na kumwaga zege kwenye miteremko mikali. Kwa sasa Halmashauri haina uwezo wa kufanya matengenezo haya makubwa kwa barabara hizi alizozitaja kutokana na fedha inazopata kwamba ni kidogo. Hata hivyo, kutokana na kiasi inachopata inajitahidi kukarabati baadhi ya barabara ili zipitike. Kati ya barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge zimo katika bajeti ya mwaka 2007/2008 ambazo ni:-

Barabara za Migilango – Tulya – Ntwike yenye jumla ya km 33 imetengewa jumla shilingi milioni 21.77 kwa matengenezo ya kawaida *(Routine Maintenance)*, Kisisiri – Kinakumi – Kiomboi km 14.4 zimetengwa shilingi milioni 9.5 na barabara ya Kiomboi – Kinalilya – Kisisiri km 9.7 imetengewa shilingi milioni 6.07 na barabara ya Kisisiri – Tulya km 18.5 imetengewa shilingi milioni 21.25 kwa matengenezo ya sehemu korofi *(sport improvement).* Barabara ambazo hali yake ni mbaya sana zinatakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa *(Construction)* na zitafanyiwa matengenezo pindi hapo fedha zitakapopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilikwishatuma maombi ya kuzipandisha daraja barabara za Shelui – Mtoa – Ndago na barabara ya Kiomboi – Kisisiri – Kidaru – Ibaga, kutokana na unyeti wa barabara hizo. Katika Kikao cha Bodi ya Barabara kilichambua maombi hayo na kupendekeza barabara moja tu ya Shelui – Mtoa – Ndago ndio ihudumiwe na Mkoa *(TANROADS).* Barabara nyingine zitaendelea kuhudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wazi na amelieleza Bunge hili Tukufu kwamba barabara hizo kulingana na hali ilivyo na jinsi zilivyo zinahitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo na ni kweli ukilinganisha hali halisi barabara hizo zinatisha sana. Sasa je, Serikali haioni haja na umuhimu wa kuongeza kupitia hiyo pesa ya *road fund* kwa mwaka huu ili barabara hizo ziweze kupitika kutokana na kiwango cha shilingi milioni 56 kilichotolewa hakiwezi kikatosheleza? *(Makofi)*

(b) Wakati akijibu swali Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja barabara ya Shelui – Mtoa - Ndago na akasema barabara hiyo ndiyo ilikubaliwa kupandishwa ili iwe barabara ya Mkoa; na kwa kuwa barabara hiyo ilitumika sana wakati wa barabara ya Sekenke ikiwa mbovu na ikawa kama barabara mbadala na kwa mwaka huu barabara hiyo haijatengewa pesa kabisa kwa ajili ya matengenezo; je, Wizara iko tayari pia kuitengea pesa ili iweze kutengenezwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza fedha kwa ajili ya barabara hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, ni kwamba fedha zinaongezwa kulingana na bajeti ya Serikali. Na barabara hizo ambazo amezitaja, barabara moja tu ambayo ameitaja kwa mfano Kisisiri-Kidaru, barabara hii ni korofi na inahitaji karibuni

shilingi milioni 600 kuitengeneza ili iwe katika hali ya kawaida. Kwa hiyo, Serikali inapanga fedha kulingana na uwezo wa fedha ambazo zinapatikana kutokana na mfuko wa barabara. Lakini hata hivyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira pindi fedha zikipatikana barabara hiyo itatengenezwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Kuhusu barabara ya Shelui-Mtoa-Ndago ni kweli barabara hii ilitumika wakati ule ambapo barabara ya Sekenke ilikuwa inatengenezwa na sasa hivi iko katika hali mbaya, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. Kwa kuwa Mkoa umeshakubali kuchukua barabara hiyo, nina uhakika mwaka ujao itapewa kipaumbele ili itengenezwe kwa kiwango kinachotakiwa.

Na. 16

**Tanzania Zanzibar Kuingia katika Ushirikiano wa Kimataifa**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa ndani ya Katiba yetu yapo mambo yahusuyo Muungano na mengine yasiyo ya Muungano; na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inashughulikia yale mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania-Zanzibar:-

(a) Je, ni kwa vipi Tanzania-Zanzibar inaweza kuingia kwenye ushirikiano wa Kimataifa kwa mambo ambayo si ya Muungano?

(b) Je, pale ambapo misaada inaletwa kwa jina la Tanzania, kwa mambo ambayo si ya Muungano Tanzania-Zanzibar inanufaika vipi na misaada hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Zanzibar inaweza kuingia kwenye ushirikiano wa kimataifa kwa mambo ambayo si ya Muungano kwa njia zifuatazo:-

(i) Inaweza kuzungumza moja kwa moja na nchi wahisani *(Bilateral Donors)* kwa miradi maalumu inayohusu Zanzibar na mfano mzuri wa hili ni kama *Submarine Cable* ya umeme toka Tanzania kwenda Pemba ambapo Serikali ilizungumza na nchi ya Norway, mradi wa maji wa mkoa wa Mjini Magharibi ambao umepatikana kutoka nchi ya Japan.

(ii) Zanzibar hushirikishwa kikamilifu katika uwakilishi wa masuala muhimu ya kimataifa kupitia mkakati wa pamoja wa Tanzania *(Joint Assistance Strategy for Tanzania)* ambao huainisha maeneo yanayoombewa misaada kwa pande zote mbili za Muungano, mfano miradi iliyokuwa chini ya *Millenium Challenge Account, World Bank, European Union* na kadhalika.

(iii) Zanzibar hushirikishwa kikamilifu katika uwakilishi wa masuala ya ushirikiano wa kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC, AU* na kadhalika.

(iv) Zanzibar hushirikishwa katika ziara za Viongozi wa Kitaifa nje ya nchi.Zanzibar hushirikishwa katika ujumbe wa Tanzania katika mikutano ya Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo *FAO, WHO, UNESCO* na kadhalika.

(v) Zanzibar hushirikishwa katika mikutano yote muhimu ya Kimataifa yakiwemo makongamano ya biashara, na mikutano ya wawekezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Tanzania inapokea misaada ya aina mbili. Aidha ya kusaidia Bajeti *(General Budget Support)* au ya miradi maalum. Kwa ile ya *General Budget Support Zanzibar* hupata asilimia 4.5 ya fedha inayotolewa kama msaada wa wafadhili mbalimbali kwa nchi yetu. Misaada inayotolewa kwa miradi maalumu haigawanywi kwani hulenga kutumika kwa miradi husika ambayo ipo pande zote mbili za Muungano.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini Mheshimiwa Waziri amezungumza kuwa Zanzibar hupata asilimia 4 tu na *point* fulani. Kama kuzingatia Serikali mbili kama Zanzibar inapata *point* 4, je, hiyo itakuwa ni sawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, mgawo wa fedha za misaada, mikopo na faida zinazotokana na Benki Kuu ya Tanzania ilipangwa kuwa ni asilimia 4.5 kwa Zanzibar na iliyobaki kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili liliamuliwa mwaka 1994 kutokana na utafiti uliofanywa na *IMF* pamoja na *World Bank.* Ni kweli kwamba kumekuwa na manung'uniko kwamba pengine kiwango hiki kimepitwa na wakati, jambo hilo linafanyiwa kazi. Tume ya Pamoja ya Fedha imeshatoa ripoti yake na Serikali mbili sasa hivi zinaifanyia kazi kwa madhumuni ya kuona umuhimu endapo upo wa kurekebisha kiwango hicho. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kama kweli Zanzibar inaweza kujiunga na Taasisi ambazo si za Muungano, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kwa nini basi Zanzibar ililazimishwa kutojiunga na *OIC* nchi ambayo ina idadi kubwa ya Waislamu hata kuliko Malawi ambayo iko katika *OIC?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, sikusema kwamba Zanzibar inaruhusiwa kujiunga na Taasisi za

Kimataifa, nilichosema ni kwamba Zanzibar inashirikishwa kikamilifu katika mikutano inayohusu Taasisi za Kimataifa. Kwa sababu hiyo naomba nirudie kwamba katika Taasisi zote za Kimataifa Tanzania inajulikana kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapana budi kwa pande zote mbili kushiriki kwa pamoja. *(Makofi)*

Ndiyo maana tunachosema ni kwamba katika mashirika ya kimataifa niliyoyataja yakiwemo *WHO, UNESCO* na kadhalika, nimesema wanakwenda kwa pamoja yaani ule ujumbe wa Tanzania unashirikisha pande zote mbili. Kwa hiyo, hivyo ndivyo itakavyoendelea kuwa na kwa namna yoyote ile Zanzibar haiwezi kuwa inawakilishwa kama Zanzibar katika Taasisi za Umoja wa Mataifa na mikutano mingine ya kimataifa kwa sababu Tanzania ni nchi moja na hapana budi twende pamoja. *(Makofi)*

Na. 17

**Uchache wa Sekondari – Tarafa ya Ngorongoro**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa ya Ngorongoro yenye wakazi takriban 70,000 na shule za msingi zaidi ya 18 ina sekondari moja tu ya Serikali; na kwa kuwa eneo lote la Tarafa hiyo ni *Conservation Area* ambapo sheria za uhifadhi wanyamapori na mazingira zinasimamiwa kikamilifu na watendaji wa hifadhi ya Ngorongoro; na kwa kuwa ujenzi wowote ndani ya hifadhi lazima *Environment Impact Assessment* ifanyike ambayo licha ya kwamba ni gharama kubwa lakini inachukua muda mrefu kukamilika na hivyo kucheleweshа maendeleo ya elimu ya Tarafa hiyo:-

((a) Je, isingekuwa busara kwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwapangia wanafunzi wanaotoka kwenye maeneo ya tarafa hiyo kwenye sekondari hiyo badala ya kuleta wanafunzi wengi kutoka nje ya Wilaya na Mkoa?

(b) Kwa kuwa nia ya Serikali ni kushawishi na kuhimiza wananchi kujenga shule za sekondari katika kila kata na angalau *high schools* moja kwenye kila tarafa, je, azma hiyo ya Serikali itafanikiwa vipi kwa maeneo yenye hifadhi kama Ngorongoro lenye sheria na taratibu ngumu za uhifadhi usiozingatia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya watu wa Ngorongoro?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Telele, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ngorongoro ina jumla ya shule za sekondari sita ambazo ni Samunge, Digodigo, Malambo, Embarway, Soitsambu na Loliondo. Shule ya Sekondari Embarway ina hosteli na ipo Tarafa ya Ngorongoro. Mwaka 2007 na 2008 wanafunzi wote waliofaulu katika Wilaya ya Ngorongoro walichaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule za Sekondari za Wilaya hiyo. Aidha, katika shule ya Embarway, jumla ya wanafunzi 168 kati ya 240 walioingia Kidato cha Kwanza katika shule hiyo mwaka 2008 wanatoka Tarafa ya Ngorongoro na wanafunzi 84 wanatoka nje ya Tarafa hiyo. Shule ya sekondari ya Embarway ni ya Kitaifa. Wanafunzi wa kutoka Tarafa ya Ngorongoro wasipojaza nafasi haizuii kuchukua wengine kutoka sehemu nyingine. Kwa ujumla katika Wilaya nafasi 34 zilibakia wazi kwa kukosa wanafunzi waliofaulu. Hata hivyo, hakuna mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule hiyo ya sekondari ya Embarway kutoka nje ya Wilaya ya Ngorongoro na Mkoa wa Arusha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na nia yake ya kushawishi na kuhimiza wananchi kujenga na kuimarisha shule za sekondari katika Kata ili kuleta maendeleo ya elimu ndani ya nchi. Hata hivyo, Wizara yangu inashauri kuwa suala la ujenzi wa shule katika maeneo yenye hifadhi kama Ngorongoro lishughulikiwe na Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na watendaji wa Hifadhi husika kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo. Aidha, Wizara pia itafuatilia ili kulielewa vizuri suala hilo. Ahsante.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imepania kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaomaliza shule ya msingi wote wanakwenda sekondari; na kwa kuwa kama nilivyosema, Tarafa ya Ngorongoro ni Hifadhi, lakini kutokana na Sheria ya Hifadhi ujenzi wa shule za sekondari hauendi kwa kasi na ujenzi wa hoteli na *lodges* zilizoko katika hifadhi ya Ngorongoro; je, Serikali inaeleza nini kuhusu hali hiyo kwamba Shule za Sekondari hazijengwi kwa sababu ya Sheria za *Environmental Impact Assessment* lakini *lodges* na hoteli za kitalii zinajengwa kila kukicha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, na hapo ndipo inastahili naona.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli kwamba katika Tarafa ya Ngorongoro ujenzi wowote lazima ufanyiwe kwanza tathmini ya mazingira. Aidha, suala hili limekuwa ni tatizo katika ujenzi wa shule za sekondari.

Hata hivyo, katika eneo la Tarafa hiyo ziko shule za msingi kama ambavyo zimeonekana katika suala hili. Na Serikali imechukua hatua ya kupendekeza kwenye Baraza la Mawaziri kwamba shule zilizoko za Msingi ziongezewe madarasa, ikama ya walimu, na utaratibu mwingine ili watoto waweze kusoma elimu ya sekondari katika

shule hizo badala ya kujenga shule zingine mpya ambazo zinahitaji *environmental impact assessments* ambazo zinachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, pili ningependa nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba hakuna hoteli ya kitalii ambayo inajengwa bila kufanyiwa *environmental impact assessment.* Aidha, ujenzi wa hoteli za kitalii ni katika hatua za Serikali za kujenga na kuboresha utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tatu ni vizuri nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba suala kama lilivyoulizwa katika sehemu ya mwisho, na mimi napenda ninukuu, je, azma hiyo ya Serikali itafanikiwa vipi kwa maeneo yenye hifadhi kama Ngorongoro yenye sheria na taratibu ngumu za uhifadhi usiozingatia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya watu wa Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii si kweli. Katika mwaka huu wa fedha Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro imetenga shilingi 1,400,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Tarafa ya Ngorongoro. Na hivyo si kweli kabisa kusema kwamba utaratibu huu hauzingatii maendeleo ya wananchi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Nyami, sasa ameingia MheshimiwaChristopher Ole-Sendeka, basi kwa kifupi atangulie Mheshimiwa Nyami, halafu Mheshimiwa Ole-Sendeka umalizie kwa sababu wewe ni jirani pale.

**MHE. PANSIANO D. NYAMI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa miongoni mwa madhumuni ya Ngorongoro ni kutunza mazingira pamoja na kuendeleza Wamasai asilia wanaoishi pale Ngorongoro; na kwa kuwa kujengwa kwa Sekondari ya Embaruwai lengo lake ilikuwa ni kupeleka watoto wa kimasai wanaoishi Ngorongoro na si kupeleka wanafunzi wengine kutoka maeneo mengine; je, ni kwa nini sasa utaratibu wa kuwachukua wanafunzi kutoka maeneo mengine ambao sio wamasai wanachukuliwa kupelekwa kwenye shule ile kinyume na utaratibu kwa sababu eneo lile ni hifadhi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyami kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitamke kwamba shule ya Sekondari ya Mbarawei ni ya kitaifa. Tukiisha iweka neno kitaifa ni kwamba inatoa fursa kwa wanafunzi kutoka mikoa mingine kujiunga pale. Hata hivyo, idadi kubwa ya wanafunzi inaanza kuchukuliwa wanaotoka maeneo yale pale. Na hii itatusaidia kujenga uzalendo, mahusiano na itatuepushia balaa la kuweka kwamba hapa ni pa wafugaji tu au wakulima tu, ni lazima tutegemeane kwa sababu wakulima ni wananchi, wafugaji ni wananchi, na wafanyakazi ni wananchi, naomba tushirikiane kuhakikisha kwamba tunaitumia shule hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi sana kuhamasisha wananchi kujenga shule kadiri zitakavyowezekana na nafasi zile zitajazwa endapo tu ufaulu utaruhusu. Kama ufaulu hautaruhusu hatutalazimika kushusha kiwango ili kuweza kuziba nafsi hizo pasipo na sababu za msingi. Asante.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Telele, amekiri kwamba *environmental impact assessment* inachukua muda mrefu; na kwa kuwa ni jambo muhimu katika eneo la hifadhi kama hiyo kufanya tathmini ya mazingira; na kwa kuwa pia Wilaya ya Ngorongoro inapaswa kwenda kwa kasi ya maendeleo katika kutekeleza sera na maamuzi ya Serikali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji, kituo cha afya kwa kila Kata, na sekondari kwa kila Kata: je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kufanya tathmini hiyo ya mazingira katika maeneo yote yanayohusika ili kutokudhoofisha jitihada za wananchi wa Ngorongoro za kujiletea maendeleo yao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika naomba kwa niaba ya Waziri wa Elimu nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika jibu nililotoa awali kwamba Hifadhi ya Ngorongoro imetenga shilingi 1,400,000,000 kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro. Ninadiriki kusema kwamba hakuna Tarafa yoyote nchini Tanzania ambayo imepewa fedha za serikali za maendeleo kama Tarafa hiyo ya Ngorongoro. Pili, maendeleo kama alivyoyasema Mheshimiwa Mbunge, hakuna mahali ambapo yamesimama ila katika hili ambalo linahusu shule, na Wizara yangu imechukua hatua stahili ili kupata kibali cha Serikali kwa kuendeleza shule za msingi ambazo ziko na zimeteuliwa kwa ajili ya kujenga shule za sekondari ili ujenzi huo uendelee bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kushirikiana na wananchi wa Ngorongoro kuhakikisha kwamba maendeleo yao hayarudi nyuma.

Na. 18

**Barabara ya kutoka Dar es Salaam – Dodoma – Singida – Mwanza kupitia Iguguno**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam – Mwanza ilikuwa inapitia katikati ya Mji Mdogo wa Iguguno ambako iko Standi ya Mabasi yanayoteremsha na kupakia abiria na mizigo; na kwa kuwa Serikali iliahidi Bungeni kuwa pamoja na barabara hiyo kutoingia Iguguno Serikali ingeweka lami ya kawaida barabara inayoingia Iguguno kutokea upande wa pili ili iungane na barabara kuu kama ilivyo kwa Mji wa Nzega na miji mingine ya namna hiyo; na kwa kuwa Serikali bado haijafanya hivyo bali

imeweka lami upande mmoja tu hivyo kufanya mabasi yasiingie na kutoka upande wa pili na kusababisha usumbufu zaidi ya k.m. 2 na mizigo yao mara nyingi usiku, na hivyo husumbuliwa na majambazi:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi yake hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna ulazima kuwekewa lami ili mabasi yaanze kuingia na kutokea upande wa pili?

(c) Kama hilo litachukua muda mrefu kutekelezeka, je, Serikali haioni kwamba kuna ulazima wa kutoa agizo na lisimamiwe kwamba mabasi yote lazima yaingie Mji Mdogo Iguguno kuteremsha abira na mizigo yao kupanda wengine na mizigo na kuendelea na safari?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira ya mji wa Iguguno, barabara ya Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia mji wa Singida ilibidi ichepushwe kidogo ili kuukwepa mji mdogo wa Iguguno kwa sababu ya usalama wa wananchi, kuepuka fidia kwa nyumba za watu na uharibifu wa mali za wananchi. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ikaahidi kujenga barabara ya kuingilia mji huo. Hata hivyo, kutokana na fedha za mkopo kutotosha mahitaji yote ya ujenzi wa barabara, sehemu ya kutoka Iguguno na kurudi barabara kuu kwa upande wa pili wa mji huo haikuweza kujengwa. Ahadi ya Serikali ya kujenga barabara ya lami kufika mji wa Iguguno iko pale pale. Serikali itatafuta fedha za kujenga sehemu ya barabara iliyobaki ya kutokea Iguguno kurudi barabara kuu kwa kiwango cha lami ili kuondoa usumbufu kwa abiria wanaoshuka au kuondokea Iguguno.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wakati Serikali inatafuta fedha za kumalizia kipande kilichobaki, ni vema uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, ukaandaa na kusimamia utaratibu utakaowezesha mabasi yote ya abiria kupitia katika mji mdogo wa Iguguno. Hatua hii ni muhimu kwa usalama wa abiria na mali zao.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa wananchi wa Iguguno wanaiamini Serikali yao: je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna umuhimu kwa mwaka ujao wa fedha, fedha hizi zitengwe ili kukamilisha kipande hicho kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu suala la nyongeza la Mheshimiwa Msindai, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, tunakubali kwamba Serikali kuanzia mwaka ujao itaanza kutenga fedha kwa ajili ya barabara hiyo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili lililopo lililojitokeza Mwanza inaonesha linaweza likajitokeza katika Wilaya ya Namtumbo kwani kuna *feasibility study* sasa hivi iliyofanyika ya utengenezaji wa barabara ya kutoka Singida, samahani, tatizo lililokuwepo barabara ndogo ya Singida linaonesha linaweza likajitokeza katika Wilaya ya Namtumbo ambapo sasa hivi katika *feasibility* waliyokuwa wanafanya kwamba barabara itapita nje ya makao makuu ya Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, sasa tulikuwa tunataka tu kufahamu kama Serikali itatenga fedha za barabara hii kuweka lami itakayoingia katika katikati ya Wilaya ya Namtumbo na kuunganisha katika barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON N. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mtaalamu Mshauri ambaye amechora barabara hiyo ya kutokea Tunduru kuja Songea kupitia Nantumbo amependekeza barabara ipite nje ya mji au makao makuu ya Namtumbo. Lakini bado hatujaafikiana na kuwa na hakika kwamba kweli barabara hiyo itabidi iwe *by pass.* Lakini ni nia ya Serikali kwamba barabara zote ambazo ni *by pass* na zinapita barabara kuu zinazopita miji husika, basi Serikali iwe na mkakati wa kujenga barabara zinazoingia kwenye miji husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kawawa, kama mwishoni tutaamua kwamba barabara ile ipite nje ya makao makuu ya Wilaya ya Namtumbo basi serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga hiyo barabara ya kuingilia Namtumbo.

Na. 19

**Vivuko vya Watembea kwa Miguu**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI (VITI MAALUM)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa idadi ya magari imeongezeka sana katika Jiji la Dar-es-Salaam hadi kusababisha tatizo la kuvuka barabara kwa wananchi wengi hasa walemavu:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za kujenga vivuko kwa waenda kwa miguu kama ilivyo Manzese?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kwamba vivuko vya watembea kwa miguu ni muhimu sana ili kuhakikisha usalama wa watembea kwa miguu, hasa watoto, wazee na walemavu sehemu za mijini ambako kuna magari mengi hasa yale yanayokwenda kwa mwendo wa kasi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ina mpango wa kujenga vivuko *(pedestrian bridges)* kumi na mbili vya watembea kwa miguu kwenye barabara mbalimbali jijini Dar-es-Salaam katika sehemu zenye matukio mengi ya ajali zinazosababishwa na wingi wa watembea kwa miguu wavukao barabara. Barabara zitakazohusishwa kwenye mpango huu ni pamoja na Morogoro, Kawawa, Uhuru, Nyerere, Kilwa, Ali Hassan Mwinyi, Bagamoyo, Nelson Mandela, Sam Nujoma na Msimbazi.

Mheshimiwa Spika, hatua za awali za ujenzi wa vivuko hivyo zikiwamo upembuzi yakinifu na usanifu wa awali zilikwisha kamilika. Hata hivyo, mpango huu ulisitishwa kwa muda ili kupisha mradi wa mabasi yaendayo kasi yaani *DART*, baada ya kuona kwamba barabara zinazotazamiwa kujengwa vivuko hivyo ziko pia kwenye mradi wa mabasi yaendayo kasi. Pia kumekuwa na umuhimu wa mradi wa mabasi kuanza kwanza ndipo vivuko vijengwe ili kupata vipimo halisi vya upana wa barabara na vivuko vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, watembea kwa miguu wengi hupendelea kuvuka Barabara kwa kufuata urahisi bila kuzingatia usalama wao. Kwa mfano, eneo la Manzese iliilazimu Serikali kujenga uzio ili kuwalazimisha watembea kwa miguu kutumia daraja lililopo. Tungependa kutoa wito kwa watembea kwa miguu kutumia vivuko rasmi vilivyoainishwa badala ya kuvuka barabara ovyo na hivyo kuhatarisha usalama wao na kuharibu mazingira na miundombinu ya barabara zetu.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza:-

(a) Je, anaelewa Waziri kwamba madereva wa magari ya Daladala pia nao huzitumia hizo njia za kupita wananchi na yupo tayari kuchukua hatua ya kuzuia suala hilo? *(Makofi)*

(b) Je, Serikali ina mipango gani kuanzisha kujenga zile barabara za juu (*flye overs)* kama nchi nyingine kutokana na kukua kwa nchi yetu na miji yetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON N. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, ningependa kumjibu Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo, lakini kwanza nimpongeze kwa maswali yake mazuri:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, Daladala zimekuwa hazifuati sheria katika kutumia barabara na katika vikao vyetu vya Bodi ya barabara katika mkoa wa Dar-es-Salaam tumesisitiza sana Jeshi la Polisi lisaidie hasa Usalama Barabarani na kwa kweli wameanza kazi hiyo. Bado hawajafanikiwa kutokomeza kabisa tatizo hilo lakini kwa hizi siku za karibuni *SUMATRA* na Jeshi la Polisi limefanya kazi nzuri ya kuwakamata madereva wa Daladala wanaovunja sheria. Serikali itaendelea kuwadhibiti ili wasipite kwenye njia za wapita kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *fly overs* katika jiji la Dar-es-Salaam, ni kweli kwamba kuna mahitaji sasa ya kujenga *fly overs.* Lakini tatizo la *fly overs* mpaka sasa ni uwezo wa Serikali. Lakini *studies* ambazo tunafanya ni pamoja na kuangalia uwezekano katika vile vivuko nilivyovisema, inawezekana kama uwezo utakuwepo baadhi yake tukajenga *fly overs.* Lakini hili litategemea uwezo wa Serikali na mipango halisi ya kuboresha usafiri katika jiji la Dar-es-Salaam.

Na. 20

**Barabara ya Kutoka Ludewa - Lupingu**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (K.n.y. MHE. LEDIANA MAFURU MNG’ONG’O)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa barabara ya kutoka Ludewa hadi Lupingu inapitia kwenye Milima mikali hivyo kufanya matengenezo yake kuwa magumu na ya gharama kubwa kwa Halmashauri ya Wilaya kuyamudu:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuifanya barabara hiyo kuwa ya Mkoa ili kuipunguzia Wilaya gharama ambazo hatuwezi kuzimudu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON N. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng’ong’o, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba vigezo vya kupandisha daraja barabara mbalimbali vimeainishwa katika Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Hivi sasa Wizara yangu inaandaa Kanuni za Sheria hiyo ili taratibu za kupandishwa na kutelemshwa daraja kwa barabara yoyote ziweze kuwa wazi zaidi. Hivyo basi, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kuvuta subira hadi hapo Kanuni za Sheria hiyo zitakapokamilika ndipo zoezi la kupandishwa au kushushwa daraja barabara mbalimbali nchi nzima litafanyika.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Asante Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza licha ya kutaka tusubiri mpaka utaratibu utakapokamilika, na kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu ugumu wa kutengeneza barabara katika Wilaya ya Ludewa, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya kutokea Mlangali kwenda Mbeya kupitia Wilaya ya Makete ambayo Mheshimiwa Rais Mstaafu Mkapa, alienda kuzindua daraja kwenye mto Yamachi miaka mingi iliyopita na kuagiza kwamba barabara ile sasa ishughulikiwe na Mkoa ili iweze kuwa kiungo kizuri kati ya Wilaya ya Ludewa kupitia Makete kwenda mpaka Mbeya kurahisisha masuala ya biashara na usafiri. Je, Wizara ina utaratibu gani kulishughulikia suala hilo ambalo ilikuwa ni maagizo ya Rais Mstaafu? Asante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa namna alivyoelezea hiyo barabara na kwa namna ninavyoifahamu ni barabara ambayo inakidhi vigezo vya kupandishwa daraja. Lakini kama nilivyosema tusubiri basi hizi Kanuni zikamilike ili taratibu sasa zifanywe za kuangalia uwezekano wa kupandisha barabara hiyo ili iweze kuhudumiwa na *TANROADS* au Wizara ya Miundombinu.

Na. 21

**Usimamizi wa Ndege za Abiria Nchini**

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na matukio ya kuanguka kwa ndege zikiwa na abiria na kusababisha vifo; na kwa kuwa ajali hizo zimekuwa zikitokana na hitilafu zinazotokana na matengenezo hafifu; na kwa kuwa hapa Tanzania zipo ndege za abiria ambazo nyingi zimekuwa zikiahirisha safari kutokana na ubovu:-

Je, Serikali inatueleza nini kuhusu usimamizi wa ndege zinazotumika hapa nchini ili kuwatoa wasiwasi wananchi kuliko hali ilivyo kwa kila kampuni ya ndege kujisimamia yenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassim, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga nchini, chini ya Sheria ya Usafiri wa Anga ya Mwaka 1977 ndicho chombo kinachosimamia masuala yote ya usafiri na usalama wa anga nchini. Hivyo mashirika ya ndege yote yanasimamiwa na mamlaka hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hizo, Mamlaka hutoa vyeti vya uendeshaji yaani *Air Operators Certificate (AOC)* kwa kampuni husika kila mwaka baada ya kujiridhisha kwamba kampuni hiyo inafanya shughuli zake kwa kiwango au viwango vilivyowekwa na shirika la kimataifa la usafiri wa anga yaani *ICAO* na pia kampuni iwe imetimiza mambo yafuatayo:-

(a) Inakidhi viwango vinavyoonesha uwezo wake wa kufanya matengenezo ya ndege.

(b) Ina marubani na Wahandisi wa Ndege wenye elimu inayokubalika, uwezo na uzoefu wa kutosha na kwamba wanafanya mitihani na kufaulu katika kiwango kinachotakiwa kwa kila ndege wanazohudumia.

(c) Ina vifaa/nyenzo za kufanyia matengenezo ambavyo vina ubora unaotakiwa.

(d) Ina miongozo ya utengenezaji ndege (*aircraft maintenance and service manuals)* iliyotolewa na kampuni mama iliyounda ndege ambayo imeridhiwa au imeidhinishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Spika, aidha kila mwaka, kila ndege hukaguliwa na kupewa Cheti cha Udhibiti wa ubora na Mamlaka *(Certificate of Airworthiness)* baada ya kuthibitisha kwamba imefanyiwa matengenezo yanayostahili kulingana na taratibu za matengenezo ya aina hiyo ya ndege yaliyoainishwa na kampuni iliyounda ndege hiyo na kuridhiwa na Mamlaka kulingana na taratibu za *ICAO.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Mamlaka hufanya ukaguzi wa kushtukiza (*adhoc inspections)* wa mara kwa mara kwa ndege, karakana na viwanja vya ndege kwa lengo la kuhakikisha kwamba usafiri wa anga unakuwa wa salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Utafiti uliofanyika kuhusu vyanzo vya ajali za ndege nchini ambazo zimetokea tangu 1997, umeonesha kuwa hakuna hata moja iliyosababishwa na ubovu au matengenezo hafifu. Ajali nyingi zimesababishwa na makosa ya kibinadamu (*human factors)* ya marubani na uendeshaji, utawala wa kampuni za ndege, miundombinu hafifu au duni ya viwanja vya ndege na hali ya hewa. Takwimu za kimataifa nazo zinabainisha kuwa tatizo hili husababisha 75% ya ajali zote za ndege na matengenezo ni 4% ya ajali zote za ndege.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya ndege pamoja na kampuni zote zilizopo nje ya nchi zifanyazo matengenezo ya ndege zirukazo humu nchini husimamiwa na Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga kulingana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa na *ICAO.* Makampuni hayo hukaguliwa kila mwaka na kupewa kibali kama nilivyoeleza cha kuendelea kufanya matengenezo. Pia kila mwaka ndege zote hukaguliwa na kupewa cheti cha udhibiti kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote kwa ujumla kwamba usafiri wa anga hapa nchini ni wa salama na waendelee kuutumia wakati wote katika shughuli zao. Aidha, Tanzania ni moja ya nchi chache Barani Afrika zenye rekodi safi ya Usalama wa Usafiri wa Anga na ni mojawapo ya nchi zlizopata hati safi ya ukaguzi ya *ICAO. (Makofi)*

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuongeza swali moja.

Kwa kuwa miaka 10 iliyopita kampuni inayotengeneza ndege aina ya *Boeing 737,* ilitoa agizo kwamba ndege zote ambazo zimeruka zaidi ya saa 50,000 zifanyiwe uchunguzi wa kina kwa vile nyaya zake za umeme huwa zinapita katika matanki yake ya mafuta na mara nyingi huwa zinapata michubuko; je, ndege zetu baada ya kufanyiwa uchunguzi huo miaka 10 iliyopita hadi leo zimekamilisha saa 50,000 za kuruka na zimefanyiwa tena matengenezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, unasoma ama?

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Hapana sisomi, nimeelekea chini. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Umeinama tu! Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na yeye kwamba kampuni ya *Boeing* ilitoa maelekezo hayo. Napenda nimhakikishie kwamba ndege za *Air Tanzania* ambazo tulizokuwa nazo, zote zilirekebishwa na zinafanya kazi kama inavyotakiwa.

Na. 22

**Biashara ya Vyuma Chakavu**

**MHE. FUYA G. KIMBITA (K.n.y. MHE. SHALLY J. RAYMOND)** aliuliza:-

Kwa kuwa biashara ya vyuma chakavu imeshamiri sana nchini na hakuna rasimu ya vyuma hivyo; na kwa kuwa hali hiyo imesababisha mifuniko ya *septic tanks,* mita za maji kung'olewa na hata vyuma vya reli kuharibu miundombinu husika na vilevile

kuhatarisha maisha ya wananchi;  je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutunga Sheria kuhusu ulinzi wa vyuma hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, biashara ya vyuma chakavu imeshamiri sana nchini hali inayosababisha mifuniko ya *"septic tanks"*, mita za maji na hata vyuma vya reli kung'olewa hali inayohatarisha maisha ya wananchi. Wakusanyaji wa vyuma chakavu wasio waaminifu wanafanya uharibifu huo kwa siri kwa lengo la kujitajirisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo Sheria ya *"The Export Control Act* ya mwaka 1962 ya kusimamia ulinzi wa vyuma chakavu na vinginevyo. Kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria hiyo, Serikali imepiga marufuku kuuza nje ya nchi chuma chakavu ambacho kinatumiwa na viwanda vyetu vya ndani vya kuyeyusha chuma kama malighafi. Lengo la hatua hiyo ni kuviwezesha viwanda hivyo kupata malighafi za kutosha kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali za chuma zikiwemo nondo, vipuri, risasi, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, chuma chakavu kilichopigwa marufuku kuuzwa nje ya nchi ni chuma na chuma cha pua (*iron & steel), alminium, brass* na *batries* za zamani za magari. Aina nyingine zote za chuma chakavu kama vile shaba, *zinc, tin,* na kadhalika vinaruhusiwa kuuzwa nje ya nchi kwa sababu havina soko la ndani kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka uwezekano wa chuma chakavu kilichokatazwa na Serikali kusafirishwa nje ya nchi na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, Serikali imeunda timu ya wataalamu ya kukagua chuma chakavu kabla hakijasafirishwa nje ya nchi.  Timu hiyo ya ukaguzi ina Wajumbe kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Usalama wa Taifa na Mwakilishi wa Wayeyushaji chuma chakavu (*smelters).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na sheria niliyoitaja kuwa ni ya siku nyingi, ni dhahiri kwamba Sheria hiyo imepitwa na wakati na inayo upungufu mwingi unaotoa mwanya kwa baadhi ya wafanyabiashara wa chuma chakavu kwenda kinyume na matarajio yaliyokusudiwa. Kwa hiyo, Wizara yangu imeanza kuichambua Sheria hiyo ili kubaini upungufu na mianya iliyopo kwa lengo la kuifanyia marekebisho ili kubaini upungufu na mianya iliyopo kwa lengo la kuifanyia marekebisho ili iweze kutumika kikamilifu kudhibiti biashara ya chuma chakavu nchini kwa lengo la kukabiliana na uharibifu huo.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini naomba niulize swali moja la nyongeza:

Kwa kuwa hii biashara ya chuma chakavu imeleta hasara nyingi sana ikiwa ni pamoja na miundombinu ya umeme na vitu vingine na barabara kuharibiwa pamoja na wizi unaoendelea. Ni kwa nini sasa tusilete au Serikali itoe agizo la kuzuia hii biashara kwa muda tukizingatia kwamba watu wanafanya hii biashara na kuiletea nchi hasara kubwa au watu binafsi hasara kubwa sana tukijua kwamba hivi karibuni imekwishatangazwa tenda kuhusu mambo ya upatikanaji wa chuma huko Liganga au Mchuchuma? Na wakati huo huo tupige marufuku kwa muda tukisubiri kwa sababu ya matumaini ya maisha mazuri tunayotarajia hapo mbele ya safari ili maisha mazuri yakishapatikana nadhani ile hali ya kuchukua chochote kwenda kuuza itakuwa imepungua.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Serikali inaendeshwa kwa Sheria, taratibu, na Kanuni. Kwa hiyo, pamoja na athari zinazoendelea kupatikana sasa hivi kutokana na biashara hii ya wafanyabiashara wa chuma wasio waaminifu, isingekuwa busara kuweza kutoa, kupiga marufuku bila kutumia taratibu za kisheria ambazo zinahitajika kiserikali. Kwa hiyo, ndio maana tumesema kwamba ni bora tuichambue hiyo Sheria ambayo inasimamia usimamizi wa biashara ya chuma chakavu ili sheria hiyo itakapokuwa imetungwa sasa ndio tunaweza tukatumia hata amri lakini kwa kufuata Sheria na taratibu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa biashara hii ya chuma chakavu inasimamiwa kwa mujibu wa Sheria, kumekuwa na maagizo yanayotolewa na wakuu wa Mikoa kupiga marufuku biashara ya chuma chakavu katika Mikoa yao; je, amri hizo zinakinzana na Sheria hii?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati kama ifutavyo:

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi hapa nimesema kwamba wale wanaofanya biashara hii, wanafanya kwa siri na kwa kweli wanavunja taratibu. Kwa hiyo, amri zinazotolewa na Wakuu wa Mikoa inapokuwa imebaini kwamba uharibifu huo upo wa kukithiri katika maeneo yao, bado unafuata taratibu kwa sababu ya nia ya kuwalinda wananchi katika kuzuia uharibifu unaoendelea katika mikoa yao.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali la nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema nchi inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu na sheria lakini ukiukaji wa sheria hizi za vyuma chakavu umekuwa ni mkubwa kiasi ambapo madaraja mengi yanaharibiwa, miundombinu ya reli inaharibiwa, pamoja na kwamba hivi karibuni wauza vyuma hawa wameangusha mpaka nguzo ya *TANESCO* na ikatuletea hasara kubwa; na kwa kuwa Mkoa wa Morogoro umekwishapiga marufuku uuzaji wa vyuma chakavu, Mkoa wa Mbeya nao umefanya hivyo, sasa ni wakati Serikali inaleta sheria Bungeni ili wauza vyuma hawa wapigwe marufuku kabisa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, hayo madhara ambayo anayataja Mheshimiwa Mbunge ndiyo hayo hayo ambayo tumeyaeleza katika majibu ya msingi na kwamba yanapokuwa yanabainika dhahiri hatua lazima zichukuliwe na ndiyo maana baadhi ya wakuu wa Mikoa wamechukua hatua hizi. Lakini ili kuwa na suluhisho la kudumu ni lazima tutengeneze sheria ambayo sasa itakuwa ni ya nchi nzima kuhakikisha kwamba usimamizi unakuwa wa jumla badala ya kusubiri mpaka wahusika wabainike kama ambavyo wanafanya katika baadhi ya Mikoa.

Na. 23

**Utekelezaji wa Hukumu ya Kunyongwa**

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR (K.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria za nchi hutungwa na Bunge kisha husainiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Sheria na kuanza kutekelezwa; na kwa kuwa moja kati ya Sheria hizo ni ile ya kunyongwa kwa wanaopatikana na makosa ya jinai, uhaini, na kadhalika lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu:-

(a) Je, kuanzia uongozi wa nchi wa Awamu ya Kwanza hadi Awamu hii ya Nne, ni watu wangapi wamekwishanyongwa na ni awamu gani iliyoridhia utekelezaji wa hukumu hiyo?

(b) Kwa kuwa utekelezaji wa hukumu hiyo umekuwa mgumu na mzito hasa kwa mamlaka ya mwisho ya kusaini hati ya kumnyonga mwenye hatia; je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa ya kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ili kuifuta adhabu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya watu 82 wamenyongwa kuanzia awamu ya kwanza hadi awamu hii ya nne. Kati ya watu hao, 10 walinyongwa wakati wa awamu ya kwanza na 72 walinyongwa wakati wa awamu ya pili. Hakuna ambaye alinyongwa wakati wa awamu ya tatu na awamu ya nne.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa adhabu ya kifo bado ni adhabu halali hapa Tanzania. Zipo nchi kadhaa duniani ambazo bado pia zinatekeleza adhabu hii yakiwemo baadhi ya majimbo ya Marekani.

Hata hivyo, ili kujiridhisha kama bado adhabu hii ni muafaka kwa wakati huu na kama inaendana na misingi ya haki za binadamu, Serikali imepanua wigo wa maoni ya wananchi kwa kuiagiza Tume ya Kurekebisha Sheria kuanza mchakato na hatimaye kutafuta maoni ya wananchi ili kuona kama adhabu hii iendelee kuwepo katika vitabu vyetu vya Sheria au hapana. Baada ya mchakato na maoni hayo, Serikali kwa kuzingatia maoni ya wananchi walio wengi itachukua hatua tahfifu dhidi ya adhabu hiyo na ikibidi italeta Muswada hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kama nilivyofanya wakati nikijibu swali Namba 195 la Mheshimiwa Engineer Stella M. Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote na kwa kupitia Bunge lako Tukufu, niwasihi wananchi wote watoe ushirikiano kwa Tume ya Kurekebisha Sheria wakati wa zoezi la kukusanya maoni juu ya jambo hili.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa tendo la kuua ni la kikatili na la kinyama; na kwa kuwa yule anayehukumiwa kunyongwa hadi kufa huwa hanyongwi hadi kufa, tendo linalompelekea kuwa duniani hayupo wala ahera hajafika adhabu hutolewa na chombo cha mahakama kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Katiba; je, isingefaa sasa Muswada ukaletwa Bungeni ambao utabainisha kwamba adhabu ya kunyongwa maana yake ni miaka 50,60 na kadhalika badala ya kumweka mtu hajui hatma yake?

(b) Kwa kuwa mauaji sasa yanashamiri kila siku kupitia sababu mbalimbali kama vile ujambazi, ushirikina, ulevi, kitu kinachoitwa hasira kali za wananchi, wivu wa mapenzi na visasi na kadhalika; je, isingefaa sasa ukawekwa mtaala wa elimu katika shule zetu za awali, msingi, sekondari ili kusaidiana na taasisi za dini kujenga taifa la wastaarabu na wenye amani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimesema katika jibu langu la msingi kwamba adhabu hii imekuwa ikitekelezwa na tayari watu 82 wamenyongwa. Utaratibu wa kufikia hatua hii ni mrefu kidogo. Mtu anapohukumiwa adhabu ya kifo na Mahakama Kuu anapata fursa ya kwanza kukata rufaa katika mahakama ya rufaani. Kisha kama mahakama ile itamwona bado ana hatia basi ipo Kamati ya Huruma ambayo inajumuisha viongozi mbalimbali na Mwenyekiti wao akiwa Rais. Kama hii inachunguza maoni ambayo yatakuwa yameletwa na mwanasheria Mkuu wa Serikali, kinachukua pia ya Katibu wa Wilaya ambapo anatoka mtu aliyehukumiwa, kinachukua pia maoni ya Jaji ambaye alitoa hukumu ile hapo awali. Basi Kamati hiyo huyachunguza maoni hayo na inatoa mapendekezo yake kwa

Mheshimiwa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Mheshimiwa Rais akiona kwamba adhabu sasa inastahili kutolewa basi huitoa. Lakini anao uhuru vile vile wa kutokuitoa. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba kwa sasa labda hawa watu 82 wanaonekana wachache lakini bado adhabu hii imekuwa inatolewa na itaendelea kutolewa katika awamu zinazokuja.

Swali la pili, kwamba makosa ya uuaji yamezidi kuwa mengi, ni kweli nakubaliana naye na ni wazo zuri kwamba pengine ni bora tukalifikiria somo lipelekwe katika shule zetu au vyuo vyetu ili tuwajenge vijana wetu katika maadili mazuri. Kwa kweli makosa yote yanayofanywa na binadamu yanatokana na udhaifu katika maadili ya watu wahusika. Kwa hiyo, ni bora tukajenga maadili mema kwa jamii yetu hasa vijana wetu wa shule.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mtazamo wa dunia nzima hivi sasa ni kuhakikisha kwamba sasa sheria hii ya kunyongwa au kunyonga inaondelewa kabisa katika sheria za nchi. Nchi nyingi hivi sasa zinatekeleza mtazamo huo. Je, Serikali haifikirii hivi sasa kuondoa adhabu hiyo na kuanza kutekeleza utaratibu mwingine ambao unafaa zaidi, maana hii ni adhabu ya kikatili na adhabu isiyofaa kwa binadamu, anayeweza kunyonga ni Mungu peke yake? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu kwa maoni hayo maana si swali. Hayo ni maoni yake.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa *comments* kwenye maoni ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi kuhusu mtazamo wake juu ya suala hili la adhabu ya kifo. Wala siyo sahihi kusema nchi nyingi zinaelekea kuifuta sheria hii kwa sababu zipo nchi nyingi pia zilizokuwa zimeifuta sasa zinataka kuirudisha adhabu hiyo.

Kwa hiyo, suala la adhabu hii kwa kweli linahitaji mjadala mkubwa maana kuna pande mbili, kuna wale ambao wamempoteza ndugu yao ambaye ameuawa kikatili kabisa na kuna wale ambao wanadhani sasa ni haki ya binadamu kumwachia huyu aliyefanya kosa hilo. Kwa hiyo, mimi nadhani mjadala huu uendelee na kama nilivyosema Tume ya Kurekebisha sheria inafanya kazi hii, inakusanya maoni, tutafika mwisho na uamuzi utakaopatikana basi tutauleta katika Bunge lako Tukufu. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 24

**Muundo wa Wabunge na Sheria Zisizo za Muungano**

**MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII)** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano limepewa mamlaka ya kikatiba kuamua masuala ya Muungano kama vile, ushirikiano wa kimataifa, Jeshi la ulinzi na mambo ya ndani ya nchi:

(a) Je, Muundo wa sasa wa Wabunge wa upande wa pili wa Muungano kutunga sheria katika Wizara ziziso za Muungano utarekebishwa lini na Serikali?

(b) Je, ni kikwazo gani kinachokwamisha kasoro hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu, ibara ya 1, Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapatano ya Muungano yameainisha kuwapo kwa Muundo maalum wa Muungano wa kuwa na nchi moja yenye Serikali mbili, yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mamlaka kamili juu ya Mambo ya Zanzibar yasiyokuwa ya Muungano na Serikali ya Muungano yenye mamlaka juu ya mambo yote ya Muungano na ya Tanzania Bara yasiyokuwa ya Muungano.

Kwa kuzingatia muundo huu maalumu, Sheria zinazoihusu Zanzibar ambazo si za Mambo ya Muungano hutungwa na Baraza la Wawakilishi, wakati Bunge la Jamhuri hutunga sheria zinazohusu Muungano na pia zinazoihusu Tanzania Bara. Hii ni kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 64(1). Ibara ya 66 ya Katiba inaelezea Muundo wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwa wajumbe wake watatoka sehemu zote mbili za Muungano. Hilo ndilo Bunge. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa utaratibu unaotumika sasa katika kutunga sheria ndani ya Bunge hili hauna kasoro na unazingatia matakwa ya Katiba yetu na mapatano ya Muungano. Kwa hiyo, Serikali haina mpango wowote kwa sasa wa kuufanyia marekebisho utaratibu huu. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu yake mazuri. Lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri akakubaliana nami kwamba kutokana na hali ilivyo hivi sasa kuna haja maalum sisi Wabunge tukawa na semina inayozungumzia Katiba yetu kwa Bunge ili kuongeza uelewa zaidi wa Katiba hiyo na kupunguza masuala madogo madogo hasa yanayoweza kuleta uchochezi katika Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba ni jukumu la kila Mbunge anapoingia ndani ya Bunge hili kusoma vitabu viwili, Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Kanuni za Bunge, siamini kwamba ipo haja ya kufanya semina kwa jambo kama hili. Tumekuwa tukilizungumza na naamini Waheshimiwa Wabunge wanao uelewa wa kutosha, basi tuisome Katiba tena na tena. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Na mimi napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu. Lakini napenda nimrejeshe kwenye swali langu la kikao kilichopita ambapo

nilipendekeza kwamba kwa nini usiwe muda muafaka kwa kujaribu kuainisha kasoro mbalimbali kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kuna baadhi ya Wabunge humu ndani wanashiriki kutunga sheria ambazo hazi-*apply* kule Zanzibar na wao wanatunga kwa ajili ya sheria za ku-*apply* huku Tanzania Bara. Je, hizi kasoro kwa nini zisitafutiwe namna ya kuweza kuainishwa na vilevile kuweza kutoa elimu endelevu kwa Watanzania wote juu ya suala la Katiba na Muungano wa Tanzania? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, katika Bunge lililopita nilijibu swali lake Mheshimiwa Dr. Chegeni Namba 133 na nilimpa maelezo ya kina kuhusu jambo hili. Kasoro zilizopo katika Muungano wetu zinashughulikiwa na Kamati Maalum ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Chegeni anafahamu na endapo kuna jambo ambalo analiona lina kasoro linahitaji kushughulikiwa basi angelipeleka katika Kamati hii na nina hakika Kamati hii kwa uzito wake italishughulikia jambo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata limefutwa na muulizaji ameniandikia kwamba amelifuta kwa sababu anazoita yeye za kiufundi. Kwa mujibu wa kanuni siwezi kulazimisha. Kwa hiyo, nakuomba radhi Mheshimiwa Waziri wa Maji umelazimika kuja kwenye sehemu ya kuanza kujibu lakini ruhusa unaweza kwenda, sasa ni zamu ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga Mbunge wa Tabora Mjini.

Na. 25

**Huduma ya Maji**

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa Kuwa Serikali iliahidi kutenga fedha kwa ajili ya vyanzo vya maji vya Chamwino – Sh 168,290,000/-, Lupaso – Sh 19,500,000/= na Mkululu Sh. 120,000,000/= kwa lengo la kuboresha hali ya upatikanaji maji kwenye maeneo hayo; na kwa kuwa mpaka sasa fedha hizo hazijapatikana:-

(a) Je, Serikali inatoa maelezo gani juu ya ahadi yake ambayo haijatekelezwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutotimizia ahadi hiyo hasa kwenye jambo linalohusu maji linawaumiza sana wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wilaya ya Masasi (kabla ya Wilaya ya Nanyumbu kuanza kujitegemea tarehe 1 Julai, 2007) iliandaa mapendekezo ya miradi kwa ajili utekelezaji katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Miradi hiyo ilihitaji jumla ya shilingi 706,777,450/=. Miradi ya vijiji vya Chiwambo, Lupaso na Mkululu iliyokuwa imekasimiwa jumla ya shilingi 307,790,000/= ilikuwa ni miongoni mwa miradi hiyo. Mradi wa Chiwambo ulikadiriwa kugharimu shilingi 168,290,000/=, mradi wa Lupaso kiasi cha Shilingi 19,500,000/= na mradi wa Mkululu kiasi cha shilingi 120,000,000/=. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichopatikana katika bajeti ya mwaka 2006/2007 kwa ajili ya miradi midogo midogo yote ya wilaya ya Masasi, likiwemo Jimbo la Lulindi ni shilingi 138,190,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa wilaya, mwezi Juni, 2007 Serikali ilituma kiasi cha shilingi 138,190,000/= kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Fedha zilizotumwa zilikuwa zimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 54,990,000/= kilitumika kutekeleza mradi wa maji wa Lupaso (Jimbo la Lulindi) kwa kuchimba kisima kimoja, kununua pampu ya kusukuma maji na kuweka mtandao wa mabomba.

Mradi wa Lupaso ulitumia fedha nyingi kuliko ilivyopangwa hapo awali (shilingi 19,500,000/=) kwa sababu ilibidi kuchimba kisima kipya baada ya kilichokuwepo kuharibika. Kiasi kilichobaki cha shilingi 83,200,000/= kisingetosha kujengea miradi ya maji ya Chiwambo wala Mkululu, kwa hiyo, fedha hizo zimetumika kwenye miradi iliyoamuliwa na wilaya. Miradi hiyo ni ujenzi wa visima 2 vya kati vyenye pampu za mkono katika kijiji cha Mpanyani na ukarabati wa visima 10 vya pampu za mkono na uwekaji wa pampu mpya 10 za mkono katika kata 2 za Lukuledi, Lisekese katika Jimbo la Masasi na katika Kata ya Chiungutwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 kilikuwa ni kidogo kuliko mahitaji yaliyopo kwenye mapendekezo ya wilaya, miradi iliyopangwa haikutekelezwa yote ikiwa ni pamoja na miradi ya Chiwambo na Mkululu. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imetenga kiasi cha shilingi 950,412,000/= kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi katika wilaya ya Masasi. Katika Jimbo la Lulindi miradi iliyopangwa kutekelezwa ni: Ukarabati wa mradi wa maji ya mtiririko Chiwambo – Lulindi, Uchimbaji wa visima virefu viwili Mitesa, Ujenzi wa mantaki 14 ya kuvunia maji mvua, ukarabati wa miundombinu ya mradi wa Chiwambo, ununuzi wa mitambo na ukarabati wa miundombinu ya Mradi wa Mkululu. Aidha, katika Jimbo la Masasi miradi itakayotekelezwa ni: Mradi wa maji Mwena Chankanguo (*Gravity*), ukarabati wa kisima cha Nanjota, ukarabati wa visima vya kati na vifupi Lisekese, ujenzi wa matanki 8 ya kuvunia maji ya mvua na kufunga pampu mpya sekondari ya Mtapika.

Na. 26

**Kuanzisha Mji wa *Millenium* Nchini**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kijiji cha Mbola-Uyui, Tabora kinajulikana kama kijiji cha *Millenium*, Chini ya utaratibu huo kijiji hicho kinapata misaada mingi ya kimaendeleo toka *United Nations* na mpaka sasa kijiji hicho kinaendelea vizuri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupata msaada wa *United Nations (UN)* ili kuanzisha "Mji wa Milenia"?

(b) Je, kwa nini Mji huo wa Milenia ambao unaweza kuanzishwa hapa nchini usiwe Mji wa Tabora ili kuharakisha Maendeleo ya Mji huo ambao bado uko nyuma sana ukilinganishwa na miji mingine?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya Milenia (*Millennium Development Goals-MDGs*), Tanzania iliteuliwa kuwa miongoni mwa nchi kumi za Afrika katika utekelezaji kijiji cha mfano cha Milenia *(Pilot Millenium Village).* Mradi wa Kijiji cha mfano cha Milenia (*Pilot Millenium Village Project*) ulianzishwa kwa lengo la kufanya majaribio kuhusu utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya Milenia. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kijiji cha Mbola kilichoko Wilayani Uyui katika Mkoa wa Tabora kilichaguliwa kuwa Kijiji cha Milenia kwa kutumia vigezo vya kijiji maskini ambacho wakazi wake wanategemea kilimo cha kujikimu (*Subsistence agriculture*) hasa kwa kutegemea mvua inayopatikana katika msimu mmoja wa mvua. Mradi huu unatekelezwa kwa njia shirikishi ambapo Umoja wa Mataifa unachangia Dola za Marekani 70 kwa mwanakijiji kwa mwaka na Serikali inachangia Dola za Marekani 30 kwa mwanakijiji kwa mwaka, ambapo mwanakijiji anajichangia Dola za Marekani 10 kwa mwaka. Kwa kuanzia mradi unahusisha kaya 100 za vijiji vya Mbola, Mpenge na Isila zenye wastani wa watu watano kwa kila kaya, lengo ikiwa ni kufikia kaya 3,000 kwa muda wa miaka mitano ijayo. Kijiji cha Milenia kinapata pembejeo za kilimo, ikiwemo mbolea, zahanati na dawa zake muhimu na vyandarua vyenye dawa ili kudhibiti malaria. Baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imekwishafanya mazungumzo na Umoja wa Mataifa kupitia Shirika lake la Mpango wa Maendeleo (*UNDP*) na kupata maelezo kwamba suala la uanzishwaji wa Mji wa Milenia linawezekana na lipo katika utaratibu ambao Umoja wa Mataifa umejiwekea, kwamba katika kila mahali penye kijiji cha Milenia basi mji ulio karibu nacho unapata fursa ya kuwa mji wa Milenia.

(b) Kwa kuzingatia kigezo cha mji wa karibu na kijiji cha Mileni cha Mbola kupata upendeleo wa kuwa mji wa Milenia, ni dhahiri kuwa mji wa Tabora unakidhi

kigezo hicho na ili kutimiza lengo hilo Umoja wa Mataifa kupitia Shirika lake Maendeleo waliupatia maelekezo Uongozi wa Mkoa wa Tabora kuandaa mapendekezo ya uanzishwaji wa Mji wa Milenia wa Tabora na kuyawasilisha kwa Waratibu wa Mpango huo nchini Marekani. Hivyo basi ni jukumu la Serikali ya Mkoa wa Tabora kuichangamkia nafasi hiyo muhimu kwa maendeleo ya Mkoa wa Tabora na Taifa kwa ujumla kwa kuharakisha utayarishaji wa mapen Umoja wa Mataifa, *New York*, Marekani. Kwa upande wa Wizara yangu, ninapenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa nasi tunatumia nafasi yetu kama Mratibu wa Mpango huo nchini kuwashawishi wahusika ili wakubaliane na azma ya kuanzisha mradi huo muhimu wa Mji wa Milenia wa Tabora. Dalili za awali zinaonyesha kuwa Mji wa Tabora utateuliwa kuwa Mji wa Milenia.

**SPIKA:** Asante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana hayo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda niungane na wewe kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana yanayoleta matumaini kwa maendeleo ya mji wa Tabora. Napenda tu niongeze maswali madogo mawili kwa uelewa wa Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri mwenye mamlaka ya Wizara hii kwa sababu sisi wana-Tabora tutarajie nini hasa chini ya mji huu kuwa wa Milenia, maana yake nini? Kuna miradi ipi ambayo itaendana na mji wa milenia? La pili ni kutaka kuelewa tu in *advance* ni michango gani ambayo wananchi wa Tabora watastahiki kutoa ili kukidhi masharti ya kuwa mji wa milenia?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri hapa Bungeni kuwa mji wa Tabora utateuliwa kama mji wa Milenia. Kama tulivyosema katika jibu letu la msingi kuna dalili nzuri, basi mji wa Milenia wa Tabora watapa mambo kadhaa, mojawapo ikiwa kusaidia kuwa na barabara nzuri, na mifereji ambayo itaondoa maji machafu ili mbu wasipate fursa ya kuzaliana katika eneo la mji wa Tabora. Lakini vilevile mji wa Tabora unaweza ukapata shule. Moja ya jambo muhimu katika mpango wa maendeleo ya milenia ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na elimu na afya. Mambo haya yote pia yatashughulikiwa, la muhimu kabisa kwa upande wetu sisi yaani wana-Tabora lazima nao wachangie kwa sababu ni mpango shirikishi, kiasi gani watachangia itategemea maamuzi ya umoja wa mataifa kwa kushirikiana na Serikali yetu.

Na. 27

**Sheria zilizotungwa na Bunge la Afrika Mashariki**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge la Afrika Mashariki limeanza kutunga sheria na kwamba sheria hizo zitatumika katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(a) Je, ni sheria zipi ambazo tayari zimetungwa na kuanza kutumika katika nchi zote wanachama?

(b) Je, utaratibu uko vipi iwapo nchi moja mwanachama inayo sheria yake ya Bunge inayogongana na sheria mpya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki?

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kuridhia sheria hizo ndani ya Bunge halali la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama chombo cha kutunga sheria Kikatiba?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu ya (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Bunge la Afrika Mashariki la Awamu ya Kwanza (2001 – 2006) lilipitisha Miswada 13 kuwa sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miswada hiyo ni kama ifuatavyo:- (1) *The East African Appropriation Acts for 2002 – 2006;* (2) *The East African Supplementary Appropriation Act, 2005;* (3) *The East African Community Emblem Act, 2003;* (4) *The East African Community Legislative Powers and Privileges Act, 2003;* (5) *The East African Community Act, 2003;* (6) *The Laws of the Community (Interpretation) Act, 2003;* (7) *The East African Community Customs Management Act, 2004*; (8) *The East African Community Standardization, Quality Assurance, Metrology and Testing Act, 2006*; (9) *The East African Community Competition Act, 2006.*

Mheshimiwa Spika, Bunge la Awamu ya Pili (2007 -2012) mpaka sasa limepitishwa Miswada 6 kuwa Sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miswada hiyo ni kama ifuatayo:- (1) *The East African Appropriation Act, 2007;* (2) *The East African Supplementary Appropriation Act, 2007*; (3) *The East African Community Customs Management (Amendment) Act, 2007*; (4) *The Summit (Delegation of Powers and Functions) Act, 2007*; (5) *The Lake Victoria Transport Act, 2007* na (6) *The Joint Trade Negotiations Act, 2007*. Kwa mujibu wa Kifungu cha 62 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Miswada yote inatakiwa kupata ridhaa za Wakuu wa Nchi wanachama ili kuwa sheria za Jumiya. Sheria zilizotungwa katika Bunge la Afrika Mashariki awamu ya kwanza zote zilipata ridhaa ya Wakuu wa Nchi wanachama na kuanza kutumika. Spika wa Bunge la Afrika Mashariki anaendelea na mchakato wa kuwasilisha sheria ambazo zimetungwa katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki awamu ya pili kuweza kupata ridhaa ya Wakuu wa Nchi. Kati ya Sheria 6 zilizotungwa na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki awamu ya pili ni sheria mbili tu ambazo zimeanza kutumika nazo ni *The East African Appropriation Act*, 2007 na *The African Supplementary Appropriation Act*, 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, panapotokea mgongano kati ya Sheria zetu na zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki kifungu 8 (1) cha Sheria namba 4 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2001 (“*the Treaty for the Establishment of East African Community Act, 2001”)* (*Act No.* 4) kinatamka kwamba sheria za Jumuiya zitakuwa na nguvu ya kisheria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia

tarehe ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Kifungu cha 8(4) cha Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, kinatamka kwamba sheria za Jumuiya zitakuwa na nguvu dhidi ya sheria zinazopitishwa na nchi mwanachama. Kwa hiyo, iwapo kuna mgongano kati ya sheria ya Jumuiya na sheria ya nchi mwanachama, nchi husika haina budi ihuishe sheria ya ndani ili kuondoa mgongano uliojitokeza.

(c) Mheshimiwa Spika, sheria zinazotungwa na Bunge la Afrika Mashariki haziridhiwi na Mabunge ya Nchi wanachama bali zinaridhiwa na Wakuu wa Nchi. Kwa upande wa nchi yetu kifungu cha 8(1) na (2) cha Sheria Na. 4 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2001 kinatamka wazi kwamba sheria za Jumuiya zitakuwa na nguvu ya kisheria na kuanza kutumika katika Jumhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa nchi zote wanachama.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa lakini naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(a) Je, kuna utaratibu gani wa wadau kushirikishwa katika kutoa maoni kabla ya sheria hizo hazijajadiliwa na kupitishwa na Bunge la Afrika Mashariki hasa ukizingatia kwamba ni kati ya sheria sita zilizopitshwa na Bunge, awamu ya pili ni sheria mbili tu ambazo zimeanza kutumika.

(b) Kwa kuwa Tanzania bado haijanufaika sana katika mpango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa katika mfumo wa biashara ya mazao ya kilimo je, kuna mkakati sasa wa kuipitia upya sheria hii ya majadiliano ya kibiashara ya mwaka 2007 (*The Treaty Negotiation Act,* 2007) ili kuiwezesha Tanzania kupata fursa nzuri ya kibiashara hasa katika mazao ya kilimo kama vile machungwa yanayotoka Muheza kwenda nchi jirani?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kushiriki wadau katika mchakato wa kutunga sheria kifungu cha 65 cha mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kinaelekeza kwamba Katibu wa Bunge wa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anatakiwa kuwasilisha Miswada ya Sheria kwa Makatibu wa Mabunge ya nchi wanachama ili kuweza kupata maoni lakini vilevile na nchi wanachama zinatakiwa kupitia vikao mbalimbali kukusanya maoni mbalimbali kabla ya kuwasilisha maoni yao kwenye Bunge na hatimaye sheria itungwe.
Kuhusu *Joint Trade Negotation Act* ya 2007 sheria hiyo inaweka utaratibu wa jinsi gani tunaweza tukazungumza kama Afrika Mashariki katika masuala mbalimbali kama ambavyo hivi sasa tutazungumza kama Afrika Mashariki kuhusu masuala ya *EPA*.

Lakini kuhusu jinsi gani Tanzania inajipanga kunufaika na biashara ndani ya Afrika Mashariki, inayotumika ni itifaki ya Umoja wa Forodha ya Afrika Mashariki ambayo inatoa fursa ya kulinda nchi Wanachama ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mfano kulinda uzalishaji wa mahindi na bidhaa nyingine na Tanzania katika sekta

hii ya mazao ya kilimo tumekuwa tukinufaika na tutaendelea kuchukua hatua za kuongeza thamani ya mazao yetu ili tuweze kunufaika zaidi ndani ya Afrika Mashariki.

Na. 28

**Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwasilisha Serikali mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa, sasa hivi imeundwa Wizara inayoshughulikia Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi kati ya wafanyakazi wa Wizara hiyo mpya wanatoka Zanzibar?

(b) Ikiwa mpaka sasa hakuna wafanyakazi wa Wizara hiyo wanaotoka Zanzibar, je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri wafanyakazi wenye uwezo katoka Zanzibar ili Wizara hiyo iwe na sura ya Kimuungano kama shughuli zake zilivyo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Mbunge wa Donge, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Wizara imekuwa na ushirikiano mzuri kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006. Ushirikiano uliimarishwa kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo mashauriano ya moja kwa moja na kuunda ujumbe wa pamoja wa kushiriki vikao mbalimbali vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kutoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano mzuri tangu uanzishwaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ushirikiano huo unawezesha kutetea maslahi ya Taifa kwa ufanisi katika Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara kwa sasa haina mfanyakazi hata mmoja anayetoka Zanzibar ila Wizara ilinufaika sana na mchango wa Wizara ya Mambo ya Nje ambayo ni ya Muungano pale iliposhikiza (*seconding*) Afisa wa ngazi za juu kutoka Zanzibar ambaye alisaidia sana katika miaka miwili ya mwanzo wa Wizara yetu.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango gani Wizara inayo katika kuajiri wafanyakazi wenye uwezo kutoka Zanzibar, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 Wizara ilitangaza nafasi za kazi 30 Kitaifa kwa ajili ya Watanzania wa kutoka pande zote mbili za Muungano wenye sifa na ujuzi katika fani za Uchumi, Biashara, Utawala na Makatibu Muhtasi. Katika fani hizo mbalimbali, waombaji kutoka Zanzibar walikuwa 9 kati ya waombaji 1,243. Wizara iliwaita kwenye usaili waombaji wote waliokidhi viwango vilivyotakiwa katika nafasi hizo bila kujali wanatoka upande upi wa Muungano. Vigezo vilivyotumika kuwaita waombaji kwenye usaili ni kiwango cha elimu na sifa zilizobainishwa kwa kila nafasi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa waliofanikiwa kuitwa kwenye usaili ni wawili (2) kati ya tisa (9) ambao waliomba nafasi za "*Senior State Attorney*" na "*Financial Management Officer Grade II*" na aliyefaulu usaili ni mmoja (1) katika nafasi ya "*Financial Management Officer Grade II*" lakini kwa bahati mbaya hakuripoti kazini alipoitwa kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara inatarajia kujaza nafasi 31 za watumishi wa kada za Uchumi, Afisa Tawala, Afisa Utumishi, Watakwimu, Katibu Muhtasi, Madereva na Wahudumu. Wizara inatoa wito kwa Watanzania wote wa pande zote mbili za Muungano wenye sifa za ujuzi, kuomba nafasi za kazi kwenye Wizara yangu mara watakapoona matangazo ya kazi katika magazeti.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na muda wa maswali umeisha. Matangazo. Naomba wageni mtakapotamkwa msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Wapo wageni wa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, ambao ni viongozi wa CCM kutoka matawi ya Fujoji na Kiombamvua katika Jimbo la Kitope nao ni kama ifuatavyo, ndugu Mwatima Abdallah Haji, ndugu Omar Makame Juma, ndugu Haji Omar na Hidaya Ramadhani Mzee, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo Wageni 52 kutoka Shirika la *HAIFA International* ambao wako hapa Dodoma kwa mwaliko wa *Saint Gasper Hotel and Conference Centre.* Ningeomba kama wapo wasimame. Hawa ndio wageni wa *HAIFA International*, karibuni sana na ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu anaye mgeni wake bwana Ahmed Abilah Mkopo ambaye ni msaidizi wake kule Jimboni, wapo pia wanafunzi 42 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Kilimatinde Mkoani Singida, karibuni sana na ahsanteni. (*Makofi*)

Sasa ni Mikutano ya Kamati. Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kuwa leo saa sita mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kuwa leo tarehe 30 saa tano asubuhi, watakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi namba 231 ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mwenyekiti wa Chama cha Maskauti hapa Bungeni, ameomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Chama cha Skaut, kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 30 Januari, saa tano asubuhi katika ukumbi namba 133, jengo la Utawala. Wale Wabunge wote na watumishi ambao ni maskauti, wanaombwa wakutane na Mwenyekiti Abdulkarim Esmail Shah, ukumbi namba 133.

Hayo ndio matangazo niliyonayo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina udhuru kidogo, kwa hiyo ninamuomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje aendelee na shughuli ambazo ziko mbele yetu.

**NAIBU SPIKA:** *Asalaam Aleikum!*

**WABUNGE FULANI:** *Waleikum Salaam!*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kazi, Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchini wa Mwaka 2007 *(The National Prosecution Service Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kikiwa ni kikao cha kwanza kwa mwaka huu wa 2008 na kikiwa kimefanyika mwanzoni kabisa mwa mwaka, kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria na kwa niaba yangu binafsi, napenda nikutakie wewe pamoja na Wabunge wenzangu heri ya mwaka mpya.

**WABUNGE FULANI:** Na wewe pia.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mungu aendelee kutulinda na kutuwezesha kutimiza majukumu yetu tukiwa na afya njema ya mwili na akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Manyara na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Hanang, kwa majonzi makubwa, kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa

Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Mheshimiwa Benedict Losurutia alikuwa Mbunge mwenzetu kwa muda mrefu na alikuwa mahiri katika kutetea maslahi ya wananchi wa Jimbo lake na maslahi ya Watanzania kwa ujumla. Umahiri wake ulijidhihirisha zaidi pale alipokuwa na hoja. Alitumia ushawishi nguvu ya hoja katika kutoa na kutetea masuala yote yaliyokuwa na manufaa kwa Taifa, alikuwa mpatanishi, mwenye upendo na alipigania umoja na mshikamano katika Mkoa wetu mpya wa Manyara. Ninawaomba ndugu wa marehemu Benedict Losurutia, wawe na subira na Mwenyezi Mungu awatie nguvu wananchi wa Wilaya ya Kiteto na Mkoa wote wa Manyara. Mungu ailaze pema peponi roho ya marehemu Benedict Losurutia, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote wa sehemu mbalimbali nchini wakiwemo wa Jimbo langu la Hanang ambao kwa siku za karibuni wamekumbwa na maafa mbalimbali kama vile njaa na kimbunga. Ningependa wafahamu kwamba tuko nyuma yao na kwamba Serikali iko pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Pangalile Rwakatare kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Sisi tuliomtangulia hapa Bungeni, tutampa kila msaada ili asijione mpweke. Ninaamini kuwa kwa kutumia vipawa alivyopewa, Bunge hili na wananchi wa ujumla, watanufaika sana na Ubunge wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, akisaidiwa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kwa kazi nzuri ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini (*The National Prosecutions Services Bill,, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini, ulijadiliwa na Kamati mnamo tarehe 21 Januari, 2008 ambapo Wabunge walio wajumbe wa Kamati hiyo walipitia Muswada huo na pia kusikiliza maoni mbalimbali kutoka kwa wadau. Mapendekezo ya wadau na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, yamesaidia sana kuboresha maudhui ya Muswada huu. Serikali imeyakubali mapendekezo mengi ya wadau na maoni ya Kamati na kuyaingiza katika Muswada kupitia jedwali la marekebisho ambalo Waheshimiwa Wabunge wameshapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini, unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini (*The National Prosecutions Services Bill, 2007).* Mapendekezo yaliyomo katika Muswada, yanalenga katika utelekezaji wa uamuzi wa Serikali kwamba shughuli za upelelezi zitenganishwe na shughuli za kuendesha mashtaka na vile vile Mkurugenzi wa Mashtaka asimamie shughuli zote za mashtaka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza uamuzi huo, Serikali imechukua hatua kadhaa kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia Bunge, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanyiwa mabadiliko kupitia Sheria ya Mabadiliko ya 14 ya Katiba ya nchi ambayo pamoja na mambo mengine imeipatia hadhi Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa ya Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 59(b);

(ii) Kuundwa kwa Kamati ya Usimamizi au kwa lugha ya Kiingereza *Sterling Committee*;

(iii) Kuteuwa Mshauri wa Kitaalam kuishauri Kamati ya Usimamizi au *Sterling Committee;*

(iv) Uchaguzi wa Mikoa sita itakayohusika na utaratibu wa kutenganisha shughuli za upelelezi na shughuli za mashtaka katika awamu ya kwanza ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza, Ruvuma na Shinyanga; na

(v) Kuandaa Muongozo wa Uendeshaji wa Mashtaka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi tano zilikuwa ni mchakato ulioanza tangu mwaka 2004 wa kutekeleza utaratibu wa kutenganisha upelelezi na mashtaka. Tarehe 13 Septemba, 2007, Baraza la Mawaziri, lilipokea taarifa ya utekelezaji kama ilivyoelezwa na likaelekeza kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa Sheria hiyo, ni hatua nyingine muhimu katika kutekeleza uamuzi wa kutenganisha shughuli za upelelezi na shughuli za uendeshaji wa mashtaka. Chimbuko la uamuzi wa Serikali ni kama ifutavyo:-

(i) Taarifa ya Tume ya Kurekebisha Sheria iliyoitwa Msekwa *Commission* ya mwaka 1977 ambayo ilichambua utaratibu wa sasa na kuona kuwa mazingira ambapo Polisi na asasi nyingine inahodhi madaraka ya kutuhumu, kukamata, kupeleleza, kuamua kufungua mashtaka na kisha kuendesha mashtaka, yanaweza kupelekea haki kutotendekea na ni kinyume na dhana ya utawala bora. Tume ilipendekeza Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka isimamie mashtaka yote nchini.

(ii) Taarifa ya Tume ya Bomani ya mwaka 1996 ambayo ilibaini udhaifu na dosari kadhaa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kwamba licha ya majukumu mazito aliyonayo, sifa zake za kuteuliwa haziko wazi, kinga yake ya kutokuingiliwa, haikulindwa kiwaziwazi na madaraka yake ya kisheria ya kuitisha majalada ya upelelezi, kumbukumbu nyingine zinazohusu kesi za jinai na kuagiza upelelezi ufanyike hayakuwekwa bayana na kwamba utaratibu wa kumwondoa madarakani haukuwekwa Kikatiba.

(iii) Uamuzi wa Baraza la Mawaziri katika Waraka namba 46/1996, wa tarehe 21 Aprili, 1997 kuhusu mapendekezo ya kuimarisha Sekta ya Sheria, ulibaini kwamba kwa vile maamuzi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yana uzito karibu sawa na maamuzi ya Majaji, *quasi- judiciary,* uhuru wa Mkurugenzi wa Mashtaka unastahili kulindwa Kikatiba kama uhuru wa Majaji unavyolindwa. Baraza pia lilibaini kuwa katika nchi nyingine za Jumuiya ya Madola, mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka na uhuru wake wa kufanya maamuzi, umewekwa Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini ulitangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 12 Oktoba, 2007 na baadaye uliwasilishwa katika mkutano wa Bunge mwezi Novemba mwaka 2007 na kusomwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huo mambo yafuatayo yamezingatiwa.

(i) Utaratibu wa kumwondoa Madarakani Mkurugenzi wa Mashtaka;

(ii) Uhuru wa maamuzi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

(iii) Dhana ya maamuzi ya Mkurugenzi kupaswa kuheshimiwa na watendaji wanaohusika; na

(iv) Mkurugenzi atahakiki uendeshaji linganifu na ufanisi wa mashtaka nchini kote kwa kutunga kanuni, kuweka taratibu *(orders guidelines or instructions)* na kadhalika kuhusu uendeshaji mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyomo katika Muswada ni kama ifuatavyo:-

(i) Utaratibu wa kumwondoa madarakani Mkurugenzi wa Mashtaka, utawekwa kisheria;

(ii) Maamuzi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Kisheria yatatiliwa nguvu za kisheria;

(iii) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na mamlaka ya kisheria kuitisha majadala ya upelelezi au kumbukumbu zozote zinazohusu kesi za jinai;

(iv) Kutakuwa na usimamizi thabiti wa shughuli za mashata katika ngazi ya Kitaifa, Mikoa na hata Wilaya;

(v) Kutenganisha upelelezi na uendeshaji mashtaka, Polisi na asasi nyingine kama *PCCB, TRA* na kadhalika watashughulika na upelelezi na Mkurugenzi wa Mashtaka atashughulikia uendeshaji wa mashtaka. Huu utakuwa ni utekelezaji thabiti wa utawala bora au kwa lugha ya Kiingereza *good governance*;

(vi) Kutakuwepo na utaratibu mpya wa kisheria wa kuendesha mashtaka kwa malengo ya kuharakisha upatikanaji wa haki;

(vii) Mashtaka ya jinai isipokuwa machache yaliyo mepesi yatafunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ili kuondoa dhana ya ubambikizaji wa kesi kama inavyodaiwa na mahabusu na wananchi wengine;

(viii) Isipokuwa tu kwa aina maalum ya kesi, watuhumiwa watafunguliwa mashtaka Mahakamani baada ya upelelezi kukamilika na baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuridhika kuwa upo ushahidi wa kutosha dhidi ya watuhumiwa au mtuhumiwa, hali hii itaondoa dhana ya kumfungulia mashtaka kila anayetuhumiwa kutenda kosa kabla ya upelelezi kufanyika;

(ix) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na mamlaka ya kisheria kutoa miongozo na nyaraka zitakazorahisisha utendaji kazi ndani ya ofisi yake na zingine anazofanya nazo kazi;

(x) Mkurugenzi wa Mashtaka atatoa sababu ya kuondoa rufaa au maombi yanayofunguliwa na mtu binafsi kwa mhusika;

(xi) Mwanasheria Mkuu atakuwa na mamlaka ya kukagua ofisi za mashtaka, kufanya tathmini ya ufanisi ili kuboresha mfumo wa utendaji kazi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

(xii) Waziri Mwenye Dhamana atakuwa na mamlaka ya kutunga kanuni kuainisha uhusiano wa Mkurugenzi wa Mashtaka na asasi zingine kwa mambo yote muhimu yenye kuboresha mfumo wa utoaji haki;

(xiii) Kutakuwa na jukwaaa la Kitaifa linalohusisha wadau wote muhimu katika masuala ya jinai litakalokuwa na dhamana ya kuboresha na kuimarisha mfumo wa utoaji haki katika mashauri ya jinai nchini kote; na

(xiv) Yapo mapendekezo hususan sehemu ya sita ya Muswada ya kufanya marekebisho ya Sheria kadhaa ikiwemo Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka, Sura ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu sita kama ifuatavyo:-

(i) Ina mambo ya utangulizi kuhusu jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika, eneo la Jamhuri ya Muungano ambapo Sheria inayopendekezwa itatumika na ufafanuzi wa maneno na misamiati;

(ii) Muswada unapendekeza masharti kuhusu kuundwa kwa mfumo wa mashataka nchini. Sehemu hii inaihusisha fungu la nne mpaka la 18 na inatoa mamlaka ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Uendeshaji wa Mashtaka ambayo itakuwa ina Mkurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Mawakili wa Serikali, waendesha mashtaka na watumishi

wengine ambao watakuwa wanateuliwa na Mkurugenzi ili kutekeleza kazi ya chombo hiki. Katika utekelezaji wa kazi zake, Mkurugenzi ataongozwa na misingi ya kutenda haki, utekelezaji wa haki hiyo na kuzuia upotoshwaji wa Sheria na maslahi ya umma;

(iii) Muswada unaweka masharti kuhusu mtu mwenye sifa ya kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Fungu la 19 linatoa masharti ya kazi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Aidha, linaainisha kuwa mafao yake yafanane na yale yanayotolewa kwa Jaji wa Mahakama Kuu. Aidha, yapo masharti kuhusu kumwondoa madarakani Mkurugenzi wa Mashtaka.

(iv) Muswada unahusu mambo ya utawala na unampa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka kuratibu shughuli za upelelezi au kumteua Wakili yeyote kufanya kazi hiyo kwa niaba yake; na

(v) Muswada unahusu mambo ya jumla, katika sehemu hii, fungu la 26 linaweka masharti kuhusu wajibu wa Mahakama kutambua mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Sehemu hii pia inaweka masharti yanayoanzisha jukwaa la Kitaifa kuhusu masuala ya jinai litakalofanyika walau mara mbili kwa mwaka. Jukwaa hilo litafanya majadiliano yatakayoboresha usimamizi na utoaji wa haki kwenye masuala ya jinai Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi waweze kufahamu vizuri Sheria hii, Serikali imeshajiandaa na imeandaa utaratibu wa kutoa elimu kwa umma. Elimu hii itatolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya hadhara, magazeti, majarida, *radio, television* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kupitia kwako, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wajadili na kisha kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchini (*The National Prosecutions Service Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, nachukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwako wewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa Jimbo la Kiteto, ndugu, jamaa na familia, kutokana na kifo cha Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto, aliyefariki hivi karibuni. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kukutakia wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, heri ya Mwaka Mpya. Ni matumaini yangu kuwa tutautumia vema mwaka huu katika kutathmini upungufu na mafanikio yoyote yaliyojitokeza mwaka uliopita kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa majukumu yetu katika Kamati zetu na Bunge kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, uliipa Kamati kazi ya kuujadili Muswada wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchini wa Mwaka 2007 kama nilivyoutaja hapo awali. Napenda kukuthibitishia kuwa Kamati yangu imekamilisha kazi hii katika kikao chake kilichofanyika Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam, tarehe 21 Januari, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuujadili Muswada huu, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Mary P. Nagu, Mbunge, Waziri wa Katiba na Sheria, akishirikiana na wataalamu wake. Aidha, katika utaratibu ambao Bunge lako Tukufu limejiwekea, Kamati ilipokea maoni ya wadau kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(Legal and Human Rights Centre)* yaliyowasilishwa na Bwana Leonard Elias, Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanganyika Law Society)* yaliyowasilishwa na Bwana Deusdedit Simbakalia na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(Tanzania Women Lawyers Association)*, yaliyowasilishwa na Bi Hilda Stuart.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Mtoa hoja, Muswada huu una lengo la kuweka utaratibu wa kusimamia na kuendesha mashtaka nchini kwa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka ili kuiwezesha Kurugenzi ya Mashtaka kutekeleza majukumu ya utoaji haki kwa kufuata misingi ya utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Kamati inaafikiana na mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu. Kwanza, mfumo huu wa mashtaka utawezesha shughuli za mashtaka kuendeshwa kwa ufanisi zaidi kwa kusimamiwa na watu wenye Taaluma ya Sheria, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo jukumu la uendeshaji wa mashtaka katika ngazi za Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Hakimu Mkazi lilikuwa mikononi mwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kadhaa kutoka kwa wananchi kuhusu ucheleweshwaji wa kesi za jinai Mahakamani na malalamiko yanayotokana na kilio cha wananchi kuhusu kubambikiziwa kesi, kutokamilika kwa upelelezi, na tuhuma za rushwa katika vyombo vinavyohusika. Hali hii kwa kiasi fulani imewafanya baadhi ya wananchi wapoteze imani kwenye vyombo vinavyohusika. Kamati yangu inatumaini kuwa Muswada huu utasaidia sana kuondoa kero zilizojitokeza.

Pili, Muswada huu ukipitishwa na Bunge lako Tukufu, utasaidia sana kudhibiti Mfumo mzima wa mashitaka nchini kwa kutumia mbinu za kisayansi zaidi ambazo

zitazionyesha mamlaka zinazohusika mipaka ya kazi zao na kuwajibika haraka pale zitakapozembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo mazuri yaliyomo katika Muswada huu, Kamati yangu inapendekeza kuwa maeneo kadhaa ya Muswada yaboreshwe ili kuongeza ufanisi zaidi.

Eneo la kwanza, linahusu dhana nzima ya uratibu wa upelelezi wa makosa ya jinai *(coordination of investigation of crimes)* kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya Utangulizi ya Muswada huu kwenye maelezo ya jumla ya maudhui ya Muswada *(long title),* Ibara za 2, 4(3), 12 na Sehemu ya IV ya Muswada hususan Ibara ya 24(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujumla wake, Ibara hizi zinampa mamlaka Mkurugenzi wa Mashitaka kuratibu upelelezi wa makosa ya jinai kwa kushirikiana na vyombo vingine vilivyotajwa katika Muswada huu. Ingawa majukumu ya Mkurugenzi ya kuratibu makosa ya jinai si mageni, Kamati inashauri kuwa ni vizuri kuwe na tafsiri ya neno "*coordination*" ili kuweka bayana mipaka ya utendaji kazi kati ya Mkurugenzi wa Mashtaka na vyombo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, katika Ibara ya 24(1), inayotamka kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na wajibu wa kuratibu upelelezi wa makosa ya jinai (*The Director shall coordinate the investigation of crimes)*, Kamati inaona kuwa Ibara hii inampa madaraka ya moja kwa moja Mkurugenzi kuratibu upelelezi wa makosa hayo na hivyo kutoonyesha wazi dhana ya kutenganisha shughuli za uendeshaji wa mashtaka na upelelezi kama ilivyoelezwa katika Muswada huu. Kamati inashauri kuwa Ibara hii iboreshwe zaidi ili kuweka mipaka inayoeleweka na kuonyesha jinsi Mkurugenzi wa Mashtaka atakavyotekeleza jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine linahusu mfumo huu wa mashtaka kutumika kwa Mikoa sita yenye rekodi za juu za uhalifu, hatua kwa hatua. Ingawa ni kweli kuwa kiwango cha uhalifu hutofautiana Mkoa mmoja hadi mwingine, Kamati inashauri kuwa kwa vile Mkurugenzi wa Mashitaka amepewa majukumu ya kusimamia mashitaka nchi nzima. Ingekuwa vizuri zaidi Serikali iangalie mambo yale ya msingi ambayo inaweza kuyatekeleza katika Mikoa sita inayohusika na kuendelea na mambo mengine ambayo inaweza kuyafanya katika Mikoa mingine kwa kutumia vyombo au watu wale wale waliopewa dhamana ya kusimamia mashitaka katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu pia unaweza kumsaidia Mkurugenzi wa Mashtaka kushughulikia makosa ya jinai yanayoweza kuibuka ghafla katika Mikoa ambayo haikutarajiwa kukumbwa na wimbi la uhalifu. Kwa mfano, Mikoa inayokabiliwa na wakimbizi huwa na kiwango cha uhalifu cha kutisha

kinachosababishwa pamoja na mambo mengine kuzagaa kwa silaha za kivita, wakimbizi waliokata tamaa ya maisha na kadhalika.

Aidha, katika utaratibu huu, kwa kuzingatia kuwa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, ni viungo muhimu vya mawasiliano na wananchi walio wengi, Kamati inashauri kuwa Wanasheria wa Halmashauri hizo wahusishwe kwa karibu zaidi katika mfumo wa mashtaka ya jinai katika kufanikisha shughuli hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa suala la haki za binadamu limepewa kipaumbele katika Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya Haki za Binadamu kama vile Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966 *(International Covenant on Civil and Political Rights)*, Tamko la Dunia la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 *(Universal Declaration on Human Rights)*, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981 *(African Charter on Human and Peoples' Rights, 1981)* na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura ya 2 ya Sheria za Tanzania, Kamati imetafakari kwa kina haki ya mtu binafsi kuendesha kesi na kukata rufaa na nafasi ya Mkurugenzi wa Mashitaka kama ilivyoainishwa katika Katiba, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania, zikisomwa kwa pamoja na Ibara za 8(c), 9(1)(a) na 10(1)(b) za Muswada huu.

Pamoja na kukiri kuwa maneno, "maslahi ya umma" (*public interest)* kama mwongozo mmojawapo atakaozingatia Mkurugenzi wa Mashitaka katika kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 8(c), yana tafsiri pana, Kamati inaona kuwa upo uwezekano kwa Mkurugenzi huyo kutumia vibaya mwongozo huo kwa kisingizio kuwa anafanya hivyo kwa maslahi umma na hivyo kumnyima haki ya Kikatiba mtu ambaye dhamira yake ilimtuma afungue mashitaka binafsi *(public prosecution)* akiamini kuwa kama angetumia utaratibu wa kawaida wa mashitaka *(public prosecution)* asingetendewa haki. Uwezekano huo unaweza kutokea wakati Mkurugenzi wa Mashitaka atakapoamua kuendesha kesi inayotokana na mashitaka binafsi kama ilivyotajwa katika Ibara ya 10(1)(b), ambapo anaruhusiwa kuendelea au kutoendelea na mashitaka ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kwamba Serikali ina taratibu zake za kudhibiti (*checks and balance*) matumizi mabaya ya madaraka, Kamati inashauri kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka atakapoamua kuondoa mashtaka yaliyofunguliwa na mtu binafsi, awe na sababu za msingi za kufanya hivyo na zielezwe kinagaubaga kwa muhusika. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa Muswada huu uweke wazi namna maslahi ya umma yatakavyodhibitiwa pindi yatakapotumika vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 27 inayoanzisha Jukwaa la Kitaifa la Mambo ya Jinai (*National Criminal Justice Forum),* Kamati inashauri kuwa wataalamu wawili wa sheria waliotajwa katika Ibara ya 27(3)(n) kuwa wajumbe wa Jukwaa hili, wachaguliwe na Vyuo Vikuu vinavyohusika. Aidha, inashauriwa kuwa idadi hiyo ihusishe pia Mawakili wenye uzoefu wa kutosha kuhusu masuala ya jinai *(practical experts).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati kwa mwaka 2008. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Mary P. Nagu, (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria na wataalamu wake, kwa kushirikiana vema na Kamati na kuyakubali mapendekezo yetu mengi yaliyouboresha Muswada huu kufikia hatua inayoonekana Bungeni. Jedwali la Marekebisho lililosambazwa, ni ushahidi tosha wa ushirikiano huo na mchango mzuri uliotolewa na Wajumbe wa Kamati wakati wa kuujadili bila kusahau mchango wa wadau niliowataja hapo mwanzo. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Rajabu H. Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Salim Y. Mohamed, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa John P. Lwanji na Mheshimiwa Nimrod E. Mkono.

Vilevile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Emanuel Mpanda, Ernest Zulu na Charles Mloka, kwa kufanya kazi zao vizuri tulipoujadili Muswada huu na kutayarisha maoni ya Kamati mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu, liujadili na kukubali kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wenzako wameiunga mkono, hii haikuwa hoja ilikuwa ni kuunga mkono tu. Sasa nitamuita msemaji kutoka Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Shoka.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasoma hii taarifa yetu ya Kambi ya Upinzani, zimeletwa *Schedule of Amendment* sasa hivi kwa hiyo nitasema kama nilivyoandika kwa sababu sijapata nafasi ya kubadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa niaba ya Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu mambo ya Sheria na Mambo ya Katiba ambapo macho yake bado hayajapona vizuri, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria wa Mfumo wa Mashitaka Nchini wa Mwaka 2007 (*The National Prosecution Service Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchini wa mwaka 2007 *(The National Prosecution Service Bill, 2007)* kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 52 (6)(c).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia za wale wote waliofiwa na wazazi wao, watoto wao na wake zao. Pia napenda kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumpoteza Mbunge mwenzetu, Marehemu Benedict K. Losurutia. Aidha, nawapa pole wapiga kura wa Jimbo la Kiteto kwa kumpoteza Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa wapiga kura wangu wote na kuwatakia kila la kheri katika mwaka huu wa 2008. Vilevile nawapa mkono wa pole kwa maswahiba yote ya kidunia ambayo wamekutana nayo, kwa njia moja au nyingine nasema Mwenyezi Mungu ndiyo muweza wa yote na yote tumuachie yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, vilevile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Getrude P. Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa Mbunge Viti Maalum kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali *(Chief Parliamentary Draftsmen –CPD)* kwa kuleta Muswada huu ukiwa na makosa machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nirudi katika Muswada wenyewe kwenye tafsiri ya baadhi ya maneno. Neno *Public Officer* halijatolewa tafsiri katika Muswada huu. Kambi ya Upinzani inauliza je, hawa nao ni lazima wawe Wanasheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama siyo lazima watu hawa kuwa Wanasheria na kwa nini kifungu cha 4(4) kinasema, nanukuu:-

*"The Director and any Officer appointed to exercise the functions of the service under this Act or any other Written Law shall have a locus standi in courts of law"*.

Watu ambao hawana taaluma ya Kisheria watawezaje kuwa na uwezo Mahakamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 7(1), nacho kinatia wasiwasi kuwa *Public Officers* wanataaluma gani? Kama tunavyosema katika Kifungu cha 4 kwamba ikiwa siyo Wanasheria watawezaje kuamua kesi au kufuta kesi yaani *Nolle Prosequi*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hicho cha saba neno "*generally*" tunapendekeza libadilishwe na litumike neno "*strict*".

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9 kinachozungumzia juu ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinasema kwamba Vituo vyote vya Polisi vinatakiwa kutoa taarifa za makosa yote yanayotajwa kwenye kifungu kidogo cha nne. Kwa kweli orodha ya makosa ni ndefu na ikiwa *Police Stations* zote pamoja na *Police Post* zote ni lazima wapeleke taarifa basi Kambi ya Upinzani inakubaliana na wadau wa *Tanganyika Law Society* kwamba Ofisi ya *DPP* itafurika na taarifa kutoka Polisi. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inapendekeza kwamba Polisi ndogondogo yaani *Police Post* zipeleke taarifa zao kwenye vituo vikubwa vya Polisi yaani *Police Stations* ili taarifa hizo zichujwe na zijulikane zitakazoweza kupelekwa kwa *DPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 14 kinazungumzia *inquest, inquest* ni ufuatiliaji wa kina wa tukio la kifo, uchunguzi. Suala hili ni muhimu sana kisheria hivyo basi Kambi ya Upinzani inasema kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka ni bora awepo mwenyewe au amtume *State Attorney* ambaye ni *senior* na mzoefu katika kazi kwa niaba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18(3), ni *redundant*. Kambi ya Upinzani inashauri kifutwe kwa sababu mambo yote yanayohusiana na kifungu hicho yameshatajwa kwenye kifungu cha 17(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 19(1), kinasema kwamba *DPP* atakuwa na hadhi sawa na Jaji wa Mahakama Kuu. Kambi ya Upinzani inauliza je, *terms* za Jaji wa Mahakama Kuu, *DPP* na *State Attorneys*, ni sawa? Ni bora *terms of service* za *DPP* zingetajwa na mchakato wa kumwondoa ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 19(3)(b) kinachosema kuwa *DPP* ataondoshwa katika madaraka yake pale atakapokwenda kinyume cha maadili *(Code of Conduct za State Attorneys,* Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi hapa kwa nini *DPP*

afuate *Code of Conduct* za *State Attorneys* na siyo *Code of Conducts* za Jaji? Kwani watu hawa wanalingana kimadaraka na kicheo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 26(a), mstari wa pili, neno “generally” lisomeke *“personally”*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha na ninashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wasemaji waliokwishaomba ni watano na kwa sababu tuna Muswada mmoja wanaotaka kuongea wanaweza kuomba.

Nitamuita sasa Mheshimiwa Pindi H. Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa George B. Simbachawene halafu Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe atafuatia.

Mheshimiwa Pindi Chana, Karibu!

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu wa *The National Prosecution Services Act* ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa ku–*declare interest,* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka.

Kimsingi, Muswada huu ni muhimu sana hasa wakati huu wa sasa na hasa ukizingatia kwamba kesi nyingi zilikuwa zinachelewa kutokana na sababu mbalimbali. Kwa hiyo, Muswada huu kitendo cha kuletwa hapa utasaidia sana kuharakisha maamuzi ya kesi mbalimbali nchini, kwa hiyo naipongeza sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Muswada huu utasaidia kuweka utaratibu wa kusimamia uendeshaji wa mashtaka nchini yaani shughuli za upepelezi zitatenganishwa na shughuli za uendeshaji wa mashtaka na kurugenzi ya mashitaka. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu sana kwa sababu shughuli hizi zilikuwa zinatumia muda mwingi sana ambapo muda mwingine badala ya kuutumia kwenye maendeleo watu kila siku wanakwenda Mahakamani kusubiri kesi unaambiwa upelelezi bado unaendelea na shughuli mbalimbali kama hizo kwa hiyo, maendeleo yalikuwa yanakwenda *slow*. Kwa hiyo, kitendo cha kuletwa Muswada huu kwa wakati huu kitarahisisha mambo mengi sana na yatakwenda kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangi kifungu cha 9 cha Muswada huu kinachozungumzia *control of prosecution*. Hapa kimsingi ninaweka msisitizo, katika kifungu cha 9(1)(d) na (c) kinachozungumzia juu ya mamlaka ya *Director of Public Prosecution* na kwa mujibu wa Muswada huu ni kwamba kutakuwepo na uwezekano wa *Private Prosecutors* ku–*prosecute* kesi mbalimbali zinazohusiana na masuala ya *criminals. Wale Private Prosecutors* ambao watakuwa wana *prosecute* ni muhimu sana *Director of Public Prosecution* akawa ana mamlaka juu yao kama ilivyoelezewa katika kifungu cha (d) na (c) ambacho kinaeleza kwamba atakuwa na haki ya ku-*discontinue at any stage before any judgment is delivered any criminal proceeding brought to the Court by another person or authority*. Kwa hiyo, hapo ndipo msisitizo wangu ulipo kwamba licha ya kwamba kuna kibali cha kwamba *any other person* anaweza akaenda kushtaki masuala ya *criminal proceedings* lakini ni muhimu sana *Director of Public Prosecution* akawa ana mamlaka kwa sababu *at the end of the day* litakapotokea tatizo lolote juu ya *rule of law or rule of justice* ndani ya nchi yetu, *Director of Prosecution* ndiye atakayetakiwa kujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nadhani hakika ni jambo la maana sana na ni jambo la msingi sana kwa sababu tunakokwenda kutakuwa na watu mbalimbali ambao watakuwa na mamlaka hayo kwa mfano *Labour Officers* watakuwa wana uwezo wa kwenda ku–*prosecute case, Tax Officers, Wildlife Officers* na watu wengine. Sasa ni muhimu sana *Director of Public Prosecution* akawa na *mandate* juu ya *case* hiyo ili *at the end of the day* kuona kwamba haki imetendeka na masuala kama hayo. Kwa hiyo, naomba niweke msisitizo kwamba hakika ni jambo la msingi sana katika kuharakisha na kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ningependa pia kuchangia katika kifungu cha 27 ambacho kinaelezea kuhusu *National Criminal Justice Forum* kwamba kwa mujibu wa Muswada huu kutakuwa na *The National Criminal Justice Forum. The National Criminal Justice Forum* imeelezwa pale kwamba itakuwa na *members* kama ilivyoelezewa katika huo Muswada kutoka A mpaka O.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana kabisa na hawa *member* wote. Lengo la hii *Forum* ambayo itakuwepo hapo ni kuhakikisha kwamba mwenendo wa *criminal justice* unakwenda vizuri. Inasemekana kwamba hii *Forum* itakutana aidha mara mbili au mara tatu kwa mwaka kutokana na hali halisi. Kwa hiyo, nakubali sana kwamba hii *Forum* ni jambo la msingi sana na kimsingi ni kitu ambacho hakikuwepo huko nyuma kwa hiyo ni muhimu sana kikawepo na kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ninayotaka kusema ni kwamba wale Wajumbe ambao wako kwenye ile *Forum* wote ni wataalamu, wengine wanaingia kwa mujibu wa nafasi zao*, by visual of their post,* mle ndani kuna *Director of Public Prosecution, The Senior Deputy Registrar, Director of Criminal and Investigation, General Intelligence* na wengine. Sasa nina nina ushauri kwa Serikali pamoja na

watalaamu hawa wote kwamba ni muhimu sana tukawa tuna watu wa kawaida ambao wataingia mle ndani kutoa ushauri, kwa lugha nyepesi tunaweza tukasema kuwepo na *Normal Civilian Personnel. (Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu katika masuala ya *criminal* wao ndiyo *beneficiary* maana mara nyingi tunapozungumzia kesi za jinai huwa zinamgusa mtu, unaweza ukakuta kesi ya mada na kadhalika ndiyo masuala ya jinai yanayohusu *individuals*. Sasa basi, tukiweka wataalamu tu katika hii *Forum* bila kuwa na *normal personnel* ambao wanaweza wakatoa mawazo na tafakari, itakuwa ni ngumu kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba watu hawa wawepo na mkiniruhusu nitoe *elements* za hawa watu ninashauri awepo mwanaume na mwanamke kama wajumbe ambao wataingia kwenye hiyo *forum*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu vipo baadhi ya vyombo katika muundo wa Mahakama kwa mfano tunapozungumza *Primary Court* pale unakuta kuna watu wanaitwa *Assessors,* kimsingi wale *Assessors* katika *Primary Court* ni watu ambao siyo watalaamu, wanaita *Learned Sisters and Brothers* yaani ni watu wa kawaida kabisa wenye taaluma tofauti na sheria lakini huwa wanakuwepo pale ili kuangalia mwenendo mzima wa kesi na shughuli za Kimahakama kama zinatendeka kwa haki. Kwa hiyo, ninaomba nitoe ushauri wangu huo kwamba ni muhimu tukawa na *Normal Civilian Personnel* katika hii *Forum* ili kuangalia *The Rule of Law and Justice* vinavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi baada ya kusema hayo, ninaomba nichukue nafasi hii kusisitiza kwamba kwa kuwa Muswada huu tutaupitisha basi *elements ya budget* ni lazima iangaliwe ili iweze kutekelezwa kwa haraka kwa muda unaostahili. Suala la *budget* katika kutekeleza Muswada huu isiwe ni kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Charles Keenja wajiandae.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla ya kuanza kutoa mchango wangu, napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe, kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia ya Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto na pia alikuwa Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Getrude P. Rwakatare kwa kuchaguliwa na kuingia Bungeni, Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii, kutoa salamu zangu za mwaka kwa wananchi wa Jimbo la Kibakwe na Mwenyezi Mungu awajaalie ili tuweze kufanya kazi na kujikomboa na umaskini katika kipindi cha mwaka huu wa 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia hasa ya Muswada huu ni kuharakisha kesi lakini pia kuleta utawala bora kwa maana ya kuepuka lawama ambazo zilikuwa zinatolewa na watu mbalimbali na wadau mbalimbali kwamba haiwezekani ukampa nafasi mtu huyohuyo akamkamata mtuhumiwa, huyohuyo akapeleleza kesi na huyohuyo aka–*prosecute* kesi. Kama hivyo ndivyo, basi nilitegemea sana kwamba katika Muswada huu ulioletwa mbele yetu kulipaswa kuwe na sehemu muhimu sana inayoeleza madhumuni haya kwa uwazi na si kama ilivyo katika Muswada huu. Niseme tu kwamba *concern* yangu kubwa itakuwa katika eneo hilo kwamba ni wapi panagawanyika kuanzia upelelezi na uendeshaji wa mashitaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nilivyosoma Muswada huu, sijaona mahali maalum ambapo panaonyesha kwa dhati kabisa na kwa uwazi kwamba upelelezi utaanzia hapa na utaishia hapa na ndipo *prosecutor* atakapokabidhiwa kuendelea kufanya *prosecution*. Nahisi kwamba pengine kuna *omission* hiyo lakini ninajua kwa kutumia *Section* ya 28 ambayo imetoa nafasi Waziri mhusika kutengeneza *regulations*, hizi *regulations* zisije zikaenda kutunga eneo hili ambalo kwa kweli tungedhani sisi kama Wabunge ni muhimu na sisi tukashiriki katika kujua kwamba *prosecution* inaanzia wapi na upelelezi unaishia wapi? Kwa sababu nina wasiwasi wa kutokea mkanganyiko wakati huyu anapeleleza na mwingine anataka ku-*prosecute* na mwingine akasema mimi hapa sihusiki kwa sababu nilikwisha kukabidhi, sasa hii inaweza ikasababisha ule ucheleweshaji ambao tulikuwa tuna wasiwasi na tunafikiria kwamba Sheria hii itakuja kuuondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee mbele zaidi kwenye *Section* (4) ile sehemu inayosema kwamba, huyu *Director of Prosecution* wa hii Sheria mpya anayekuja kuleta hii *service*, atasaidiwa na *other officers*, lakini kwenye tafsiri kwenye ile *Section (3)* haijasema hawa *other officers* ni watu gani, kilichoelezwa pale ni kuhusu *law officers*; sasa sijui kama hawa *other officers* ndiyo *law officers* au ni *officers* wa namna gani? Hii inaweza kutuletea mapungufu katika ufanisi kama tulivyotarajia, kwa sababu huyu *Director* kwa kweli anahitaji kusaidiwa na watu ambao ni *legal officers* au *law officers* na siyo *officer* yeyote yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema kwamba, Sheria hii kama kweli kwa kadri ilivyotengenezwa hivi, kwa uzuri wake huu ambao ninauona na kwa kweli itaweza kufanya kazi katika maeneo ya majaribio kama ilivyoelezwa na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, inaweza kutusaidia. Ninapata wasiwasi pale ambapo nimesema katika hoja yangu ya kwanza kwamba, ni wakati gani hawa watu wanaachiana, maana yake utaratibu uliokuwepo toka siku za nyuma ni kwamba, ilikuwa Polisi kwanza wanakamata, wanapeleleza, wakishamaliza wanamkabidhi *Prosecutor*, *Prosecutor*

anaendelea, lakini sasa hizi zinakuwa ni idara tofauti. Pia kuna wakati ambao huyu *Director* amepewa wajibu katika sheria hii kwa ku-*coordinate investigation*, sasa anapo-*coordinate investigation* ni wakati gani ana-*coordinate*;ana-*coordinate* kwa kuwa upelelezi ulioletwa na Polisi haujakamilika vizuri, haumsaidii kuendesha kesi au ana-*coordinate* namna gani? Nayo hii pengine ningependa nipate ufafanuzi pengine ungeweza kusaidia nikaelewa, lakini ninaona kama kidogo kuna mchanganyiko katika eneo hilo la *coordination of investigation* itakayofanywa na *Director*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nilikuwa nime-*observe* maeneo hayo mawili. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa nami ya kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka *(The National Prosecutions Services Bill)*.

Mimi kwa kuanzia, siipongezi Serikali kwa sababu Muswada huu umechelewa sana na umechelewa kwa sababu mapendekezo ya awali kabisa kwa Serikali kuweza kutenganisha haya majukumu mawili ya kupeleleza na kuendesha mashtaka, yalitolewa miaka 31 iliyopita na Tume ya Msekwa *(The* Msekwa *Commission)*, lakini kwa kirefu ilikuwa inaitwa *Judicial Service Review Commission*. Sasa yanapokuja kutokea mabadiliko miaka 31 baadaye, sina sababu yoyote ya kuipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya Polisi kufanya mambo yote peke yao, tena ni matano siyo mawili au matatu kama ambavyo nimesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, maana Polisi huyo huyo anakamata wahalifu, anapeleleza matukio ya jinai, anahoji watuhumiwa *(interrogation)*, ana kazi ya kuamua je, hiyo kesi aifikishe Mahakamani au la na mwishoni huyo huyo aendeshe mashtaka. Madhara yake ni makubwa, tulifika mahali ambapo mfumo wetu wa uendeshaji masuala ya jinai *(administration of criminal justice)*, ilionekana ya kipolisi polisi na kuifanya haki isionekane kutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki isitendeke tu bali vilevile ionekane inatendeka, *justice should not only be done, should also be seen to be done*. Utaratibu huu tulionao sasa hivi ambao tunasema tunashukuru kwamba tunaondokana nao, hatukujitakia bali ulitokana na hali halisi baada ya uhuru kwamba, tulikuwa hatuna wataalam wengi wa sheria, ndiyo maana *DPP* kwa madaraka aliyonayo chini ya Sheria ya Uendeshaji Mashtaka, ikabidi sasa awateue Maofisa wa Polisi kuanzia ngazi ya *Sub-inspector* siku hizi wamebadilisha vyeo vyao na kuendelea juu kuwa *Public Prosecutors*, kwa kweli hali haikuwa nzuri. Ukisoma ripoti ya Tume ya Msekwa, walifanya utafiti Mkoa wa Mwanza ambako kulikuwa na *State Attorneys* watano tu mkoa mzima wakimsaidia *DPP* na wakiwa na jumla ya mafaili ya kesi 1474 ilikuwa miaka ya 70 hiyo.

Ukipiga wastani kila Wakili alitakiwa kuwa na mafaili 265 ya kesi, sasa kwa vigezo vyovyote vile, ufanisi hauwezi kutokea hapo. Kwa hiyo, ninasema Muswada huu unaturejesha kwenye utawala sahihi wa sheria, utawala sahihi wa kuendesha mambo

yetu, kwa sababu Bunge hili halijawahi hata siku moja kutunga sheria inayowateua Askari Polisi kuendesha mashtaka au kufanya kazi za kisheria namna hiyo hapana.

Sheria zote zilizotungwa na Bunge hili zinawapa Polisi majukumu maalum ya kipolisi, kulinda amani, mali, kuhakikisha kwamba vitendo vya jinai havitokei, kupeleleza vitendo vya jinai na kadhalika, lakini hili la sheria nao kuwa *interpreters* wa *law* na kuendesha mashtaka, liliongezewa tu na madaraka ya *DPP* mwenyewe chini ya Sheria ya Uendeshaji Mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee mambo mawili, matatu, niliyoyaona kwenye Muswada huu moja kwa moja; ni marekebisho madogo ambayo ningemwomba mtoa hoja ayazingatie akiwa na mantiki yake. Ukurasa wa 29 wa Muswada huu, kuna *clause ten* inasema, *notwithstanding the provisions of any other law relating to appeals, revisions or applications shall be the function of the Director to institute conduct and defend criminal proceedings*. Mimi neno *defend criminal proceedings,* ninaona kama lipo *misplaced,* ninaomba waliangalie tena, linaharibu kabisa kabisa mtiririko na maana halisi ya hicho, *how can you defend criminal proceedings*? Hilo neno waangalie namna ya kulipachika, *otherwise* waliondoe kabisa. Vilevile ukiangalia (b) ya hiyo *clause ten,* ninaona madaraka anayopewa tena *DPP* yanakuwa makubwa mno na ninaungana kabisa na Mwenyekiti wa Kamati aliyekuwepo hapa kwamba ni makubwa na *safeguards* zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata sasa hivi na mimi *schedule of amendment* ya Mheshimiwa Waziri kuhusu kifungu hicho hicho cha kumi kuwa, *DPP* anapochukua rufani au kesi yoyote kutoka kwa mrufani, basi itabidi atoe sababu kwa mrufani. Mimi ninaona bado haitoshi, tupo katika kipindi ambacho uhuru wa mtu lazima uwe mpana zaidi. Ninapendekeza kiongezwe kifungu kusisitiza kabisa kwamba*, in the exercise of the powers under the Act, the DPP shall have regard to the interest of justice and need to prevent abuse of the legal process,* ninachoogopa *DPP* ni binadamu pia, anaweza kutumia madaraka vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 33 wa Muswada huu kuna *sub-clause five* ya *clause* 19 inasema: "*The Tribunal shall consist the Chairman and two other persons nominated on the advice of the Attorney General from among persons who have hold the office or could have qualified to be appointed a Judge of a High Court or a Court of Appeal.*" Hii matumizi ya *article* (a), yanajenga *presumption of a broader choice of tribunal members* kutoka pengine hata nje ya nchi, lakini mimi ninavyojua hapa tunaongelea *members* waliotokea humu humu ndani na tuna *High Court* moja na *Court of Appeal* moja. Kwa hiyo, matumizi ya *article* (a), yasingefaa hapa, ninafikiri tutumie *a definitive article* ya *the,* tuseme *to be appointed a Judge of the High Court or of the Court of Appeal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini yake *part four - Administration Provisions.* Madaraka chini ya sehemu hii ya kuteua *PPs,* ninapendekeza kuwa katika ku-*exercise powers* zake hizo, *qualified Police Officers* ambao wamekuwa wanafanya hii kazi ya *prosecution* kwa miaka mingi, waweze kuhamia Ofisi ya *DPP* na ukurasa wa 35 ibara ya 27(3)(d) sijui kama imesahihishwa hiyo, ninaona hapa *members of the forum* yupo mtu

anaitwa *the Director of General Intelligence*, mimi sijawahi kumwona sijui ni nani? Panahitajika masahihisho hapa, aidha *may be the Director General of Intelligence or Director of Intelligence Services*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa neno moja tu kwamba, Muswada huu unawaongezea kazi vijana wetu Mawakili wa Serikali na kuwa-*expose* kwenye hatari kubwa zaidi. Ninasema hivyo kwa sababu mimi mwenyewe kama Wanasheria wengine wote hapa, tumewahi kupitia kuwa Mawakili wa Serikali, tunaelewa kazi yenyewe ina maana gani. Ninavyojua mimi Wakili wa Serikali ni mtumishi ambaye wajibu wake mkubwa katika utawala wa sheria haujatambuliwa sawasawa mpaka sasa. Nitatoa mifano michache tu; Wakili wa Serikali *uniform* yake ni suti nyeusi, shati jeupe na kiatu cheusi. Akishavaa nguo hizo nyeusi, anategemea mafaili yake aweke kwenye mkoba mweusi na sio kwenye mfuko wa rambo.

Huyu ni mtu ambaye anatarajiwa katika uvaaji wake anakwenda Mahakamani, atembee kwa mguu au apande daladala na mafaili ya Serikali, inatakiwa atumie *taxi* au gari. Niishie tu hapo, lakini huyo anapata Sh. 300,000, mimi ninavyojua mpaka sasa, ndiyo maboresho makubwa yaliyofanyika. Sh. 300,000 kwa mwaka kwa ajili ya nguo, sasa mimi sihitaji kuwa mtabiri kuelewa Sh. 300,000 kanunua vitu vyote hivyo, nina wasiwasi vijana wetu wanakwenda kwenye mitumba ili kupata hizo suti, maana utavaaje suti moja, kila siku upo Mahakamani na ndiyo *uniform* yako, unahitaji angalau uwe na suti tatu au nne hivi. Ninadhani haitoshi Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mshahara wa Wakili wa Serikali ni Sh. 323,390 ninavyojua. Ikikatwakatwa vijana wetu hawa wanapata Sh. 228,000. Huyu ni Wakili wa Serikali, ndiye anapambana na mafisadi Mahakamani, huyu ndiye anapambana na Mawakili wengine wanaolipwa kesi moja tu Sh. 150 au 200m, mshahara 220,000/=. Huyo kijana anatakiwa ajiandae na kesi na mara nyingi wanaondoka na mafaili kwenda kufanyia nyumbani, atapanda daladala na mafaili ya Serikali anarudi ofisini na daladala, hakuna hata *minibus* ya kuwabeba kuwapeleka kazini na kuwarudisha. Hali ya Mawakili wa Serikali ni mbaya na ningeomba Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, tusiwarundikie tu kazi vijana, lakini tuangalie na maslahi yao yakoje ili waweze kufanya kazi bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali wanapokaa hakuna anayejali. Mimi nilidhani hawa ni vijana ambao tungewaingiza kwenye kundi moja na Askari Polisi, Wanajeshi na hata watu wa Usalama wa Taifa. Leo tunawarudisha chini zaidi kusimamia kesi kwenye Mahakama za Wilaya na kwenye Mahakama za Hakimu Mkazi, kwa hiyo, *contact* na wananchi wa kawaida ni kubwa zaidi, anakaa Manzese, kuna kesi zaidi ya hamsini anazisimamia pale, watachinjwa hawa. Tuanze kufikiria leo wanakaa wapi, usafiri wao ukoje, *otherwise* mabadiliko haya hayatakuwa na maana tusipoyazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa kuwa kifungu cha kwanza cha Sheria hii kinampa madaraka Waziri kutangaza *commencement date*. Ningeomba Mheshimiwa Waziri asitangaze *commencement date* ya Sheria hii kabla hujaboresha angalau mazingira ya kufanyia kazi ya hawa vijana Mawakili wetu. Kwa mara ya

kwanza, tufanye vitu kwa usahihi kabisa badala ya kujaribu jaribu, *otherwise* itatangazwa *commencement date* mabadiliko tunayapitisha hapa, *impact* itakuwa sifuri katika jamii, kwa sababu haya mabadiliko yatafanywa na vijana ambao wana njaa, hawana usafiri, wananunua makoti yao kwenye mitumba, wanapambana na Mawakili wenye pesa huko, hata kwenda Mahakamani wanaomba *lift* kwa Mawakili wenye pesa, hapa mbele anakaa kaka yangu ni Wakili mmoja mzito, bei kali, sasa watafikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyoyasema, nitategemea sana Mheshimiwa Waziri ayazingatie. Ninaomba kuunga mkono hoja. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Bahati nzuri Wakili wa bei kali yuko humu humu ndani, kwa hiyo, anaweza kujitetea. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa John Cheyo ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache. Ninaomba nianze kwanza kwa kukiri kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo nilipata nafasi nzuri ya kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niungane na wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ndugu na jamaa wa marehemu Mheshimiwa Benedict Losurutia, aliyekuwa mwenzetu katika Bunge hili na ambaye ametangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu, awape nguvu ya kustahmili msiba huu mzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kusema, amesema Muswada huu umechelewa sana nami naomba nikubaliane naye. Afadhali kufika mahali sasa ucheleweshaji ule ukasimama, kwa hiyo, tunampongeza Waziri ambaye amekuwa katika Wizara hii kwa miaka ninafikiri miwili sasa kwa kutuletea Muswada huu ili kurekebisha hii hali iliyopo ambayo siyo nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo tulionao sasa hivi ni mfumo wenye uwezekano mkubwa sana wa kumwonea hasa mtu mnyonge, maana anaweza kukamatwa na Polisi, akatiwa mahabusu, akafikishwa Mahakamani, Mahakamani anatakiwa awekewe dhamana, hana dhamana, anakwenda kusota rumande na wapo watu ambao wamekaa rumande kwa miaka wakisubiri kesi zao zisikilizwe, wakati hata pengine kosa lenyewe hawakufanya wala hakuna ushahidi unaoonyesha kwamba wamefanya kosa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni utaratibu ambao unavunja haki za msingi sana za Watanzania na mimi ningependa kwa kweli tufike mahali tabia hii ife. Mtanzania afikishwe mahakamani baada ya kuthibitika kwamba, ana makosa ambayo yanatakiwa aende kujibu na ndiyo kazi tunayosema kwamba, *DPP* akafanye. *DPP* ataridhika kwamba kwanza, kuna ushahidi kabla ya mtu kupelekwa Mahakamani, *DPP*

ninamtegemea ataharakisha Polisi maana watampa taarifa kwamba, wana kesi wanazoshughulikia, ataharakisha kufanya upelelezi ili ukamilike, mashtaka sasa yaweze kupelekwa mahakamani na kwa hiyo mtu huyu aweze kuwekwa katika utaratibu huo wa dhamana, ambao unaweza kumpeleka ndani au akiwa na pesa aweze kulipa. J

Jambo hili linasikitisha zaidi, kwa sababu wale wenye fedha hawaendi mahabusu, wanalipa dhamana, kwa hiyo, wanakwenda nyumbani, wasiokuwa na fedha, wale maskini, ndiyo wanaopelekwa mahabusu na ndiyo waliojaza magereza yetu hivi sasa. Tungeomba sana hili libadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo na utaratibu wenyewe utakavyokuwa, lakini hilo ndiyo maana tuna Wizara, Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataangalia jinsi utaratibu huo wa upelelezi utakavyokuwa mpaka kutufikisha kwa huyu mtu kupelekwa mahakamani na katika Muswada huu, kifungu cha 28 kinampa Waziri uwezo wa kutunga *regulations* za kusimamia utaratibu huo utakavyokuwa. Tunaomba alizingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetangulia kusema kuna watu wengi sana wanasota kwenye magereza yetu hivi sasa, wakisubiri kesi zao ambao pengine nyingine hata ushahidi haupo. Sasa ningeomba mara Muswada huu utakapokuwa Sheria, *Director* wa *Public Prosecution,* aweke utaratibu utakaomwezesha kupitia haraka mashtaka yanayowakabili hawa watu wetu walioko huko Magereza ili wale ambao hakuna ushahidi wa kutosha kuendelea kuwaweka magereza, waweze kuachiwa huru maana hakuna hata fidia watakayolipwa maskini hawa ni kwamba watapata tu uhuru wao, warudi tena katika jamii wakajenge Taifa hili. Sasa hivi tunaambiwa mahabusu wanakaribia kulingana na wafungwa kwenye magereza yetu. Ninafikiri hili ni jambo la ajabu sana, ambalo inabidi lirekebishwe haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote waliozunguza, wamezungumzia madaraka anayopewa *DPP*. Madaraka ya kuamua kupeleka kesi Mahakamani ama kutokuipeleka Mahakamani. Tulisema katika Kamati kwamba ni vizuri pale atakapoamua kutokupeleka kesi Mahakamani atoe sababu. Tulielezwa kwa kirefu sana kwamba, kuna utaratibu katika Ofisi ya *DPP* unaomfanya ashauriane na wenzake kabla ya kufanya uamuzi huo, lakini hayo ni mambo ya ndani ambayo si utaratibu uliowekwa kisheria. Utaratibu lazima uwekwe utakaohakikisha kwamba, hapati madaraka tu ya ku-*withdraw* kesi Mahakamani anavyoamua ku-*withdraw*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kifungu cha 10(d), kinampa uwezo wa kuondoa hata mashtaka ya mlalamikaji Mahakamani. Katika *amendments* ambazo tumechelewa sana kupewa kimerekebishwa kidogo lakini pale mlalamikaji atakapokataa kwamba malalamiko yake yasiondolewe Mahakamani, aendelee na malalamiko yake. Labda mtu wangu ameuawa, nikaenda Mahakamani kukata rufaa kwamba siridhiki na hatua zilizochukuliwa, *DPP* anakuwa na mamlaka za kwenda Mahakamani na kuiondoa kesi hiyo hata kama mimi siridhiki na kuondolewa na kesi hiyo, ninafikiri hiyo siyo haki. Mtu ambaye ameamua kukata rufaa, aruhusiwe kuendelea na rufaa yake mpaka rufaa hiyo imalizike, ikishamalizika kama atashindwa Mahakamani, basi atakubaliana na

uamuzi wa Mahakama lakini si uamuzi tu wa *DPP* kwamba ameamua kesi iondolewe basi iondolewe. Ninashukuru sheria inatambua kwamba, mtu binafsi anaweza kuendesha mashtaka ya kesi ya jinai Mahakamani pale ambapo haridhiki na uamuzi ambao amepewa. Tungeomba sana hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ambalo ningependa kulizungumzia kwa ufupi kabisa ni kwamba, tunaambiwa kwamba utaratibu utakuwa ni kuanza na mikoa sita ambayo ina kesi nyingi za jinai. Dar es Salaam *of course* itakuwa ni kinara kama kawaida na Mwanza na Arusha, lakini haya mambo ambayo ninazungumzia ya uendeshaji wa matatizo ya kesi na watu kuonewa na watu kuwekwa mahabusu unafanyika nchi nzima. Kwa hiyo, tunaomba *DPP* atakapoanza aangalie ni mambo gani yanayoweza kufanyika mara moja katika nchi nzima na hayo yafanyike katika nchi nzima. Yale ambayo yana mahitaji maalum, basi hayo ayafanye katika mikoa sita, akijiandaa kupanua wigo wake kwenda katika mikoa hii mingine, maana kesi zinaendelea Mahakamani katika ile mikoa mingine kumi na tano, siyo kwamba tunafika mahali tunasema kwamba, sasa ninyi mikoa kumi na tano simameni tuendelee na mikoa sita. Katika mikoa ile kumi na tano mashauri bado yanaendelea, basi yaendelee chini ya utaratibu huu ambapo kwayo mtu hapelekwi mahakamani mpaka ushahidi umetosha wa kumpeleka mahakamani na *DPP* ameridhika au mwakilishi wake ameridhika kwamba, ushahidi uliopatikana unatosha kumpeleka huyu mtu mahakamani.

Kwa hiyo, tunaomba katika ile mikoa mingine, mfumo huo wa uendeshaji wa mashtaka uanze mara moja usisubiri, maana hakuna kitu kinachosubiriwa. Jukumu la kuendesha mashtaka ni la *DPP*, aanze kulitekeleza katika mikoa yote mara moja, asingoje mpaka baadaye, maana hakuna analongoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache ya kuzungumza kwamba, ninakubaliana na huu utaratibu, tunaomba Mheshimiwa Waziri akamilishe suala hili mapema na atangaze kuanza matumizi ya Sheria hii mapema iwezekanavyo. Haya mengine yanayopendekezewa, tunaomba ayazingatie pia kwa sababu kama maslahi ya watumishi wa *DPP* yatakuwa ni ya ovyo, watakula rushwa, watafanya kazi zao ovyo ovyo, yatakuwa ni matatizo mengine, tumehamisha tu kutoka Polisi tukapeleka kwa *DPP*. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba, mazingira yanayowekwa ni ya kuwafanya watumishi hawa wafanye kazi zao kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwanza kabisa, ninataka kuungana na wenzangu waliotoa pole kwa kifo cha ndugu yetu, Marehemu Benedict Losurutia, kwa niaba ya Wananchi wa Bariadi, ninatoa pole nyingi sana. Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niungane na wenzangu, waliompongeza Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge. Mimi nina matumaini makubwa kwamba, ataongeza mazuri zaidi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninataka kutumia pia nafasi hii kuwapa pole Wananchi wa Bariadi, Kijiji cha Nyamalapa kwa kukumbwa na kimbunga. Ninamshukuru sana Diwani Namazubu kwa kuweza kunitaarifu na mimi kufika mapema ili kujaribu kusaidiana na hao wananchi na pia naipongeza Wilaya kwa kufanya lolote lile ambalo limeweza kuwasaidia wale walioathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakwenda kwenye Muswada. Muswada huu matumaini ya wengi ni kwamba, utapunguza adha ya kuwa mahabusu kwa muda mrefu. Nimesoma Muswada nikiangalia ninaona umuhimu unawekwa zaidi kwa kesi ambazo ziko Mahakamani, lakini mahabusu waliopo wengi ni wale ambao wamekamatwa, wapo ndani hata mahakamani hawajakwenda. Kwa hiyo, hili tatizo ninaona bado litaendelea ni kama vile katika nchi yetu upande mmoja unataka kupunguza mahabusu lakini upande mwingine unafanya kama vile ni kazi yake ya kutengeneza mahabusu siku hadi siku. Nami ningeshauri kwa wakati huu ambapo Serikali imeamua kuwa na utawala bora, utawala wa sheria, basi tuangalie vyanzo vya mahabusu, tuangalie ni watu gani ambao wanajaza magereza yetu.

Ningependa kusema kwamba, labda sheria ambayo inasimamia nani ni mlinzi wa amani na madaraka ambayo wamepewa *DCs, VEOs* na *WEOs*. Madaraka haya yangeangaliwa kwa sababu inavyoonekana ni rahisi mno kuwaweka watu ndani na ni rahisi mno kwa watu kukaa ndani ya mahabusu kwa muda mrefu na ukija kuangalia baadaye unakuta kwamba, hakukuwa na sababu hata kidogo kwa mtu huyo kuweza kukaa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tumeanza kushuhudia kwa sababu tumepata TAKUKURU kwa mfano, nao wameanza kuweka watu ndani na baadaye wanakuachia. Mtu anaweza akakuta tu mna kabaraza kadogo mnazungumza, wanasema kwamba ninyi hapa mnazungumzia rushwa, mnakwenda ndani. Bado sasa hivi kunakuwa pia na watu wengine wanakamatwa kwa ujumla kijiji kizima mnawekwa ndani. Mimi ninasema kama hatutadhibiti uwekaji watu ndani, sheria hii haitatusaidia kwa sababu ni watu wengi mno wanapelekwa, wanakaa na huyu *DPP* ambaye tunasema sasa atasaidia, yeye anaonekana tu kule Mahakamani, lakini kuingia kule na kuona ni mahabusu wa namna gani waliopo kule na kuwatoa, haijasisitizwa na sheria hii. Ninajua kuna kipengele ambacho kinasema kwamba, anaweza akaenda gerezani lakini hakisemi atakuwa na *powers* gani na atafanya nini zaidi kwa watu ambao hawajaingia Mahakamani.

Kwa hiyo, mimi ninashauri kabisa Serikali kama kweli imeamua kutenda haki, basi jambo hili la watu kukamatwa bila kufanyiwa utafiti, ninaona lingekoma. Sasa hivi kuna kesi mbalimbali, sasa tunazungumzia juu ya Benki Kuu, tunasema hakuna aliyekamatwa kwa sababu tunangoja watu waweze kufanya upelelezi. Sasa kama hii kwa hapa juu inawezekana, kwa nini kule chini tunakimbilia tu kila wakati kamata weka ndani, hii haitatusaidia kupunguza mahabusu katika Magereza yetu, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, mpaka hivi sasa sijaona uhusiano juu ya muda ni muda kiasi gani mtu anaweza akabaki *under investigation*. Kesi inaweza kuruhusiwa kuendelea kwa muda gani? Hali hii inaweka watu katika wasiwasi kila

wakati na pia inakuwa chanzo cha rushwa na zaidi mtu akiwa Mahakamani. Haya mambo kwa sisi Wabunge imekuwa ndiyo kazi yetu, kazi ya Mbunge ni maendeleo lakini kazi kubwa sasa ya Mbunge ni kila siku mtu unapigiwa, watu wawili watatu wako ndani, Mheshimiwa tunaomba laki tano ili tutoke. Vitu hivi ni vya kawaida kila siku na mtu anaweza kukaa miaka miwili, mitatu, hata minne. Mimi ningependa kuona kuna muda unatajwa kisheria, mtu anaweza akawa *investigated* kwa muda gani, mtu anaweza kuwekwa mahabusu na akakaa kwa muda gani ili adha hii ya kujaza mahabusu katika Magereza yetu iweze kupungua na pia haki iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye Sheria kwamba, utaratibu huu utahusu Mahakama ya Wilaya, *Magistrate Courts* na kadhalika. Ninataka kuwaambia, kwa sisi ambao tunatoka kwa wananchi kama Wabunge, haki haitendeki vizuri katika Mahakama ya Mwanzo. Sijaona kama kuna uhusiano wa haraka ambapo watu wanaweza wakatolewa kule ambako yule Wakili hafiki wakafika kwenye Mabaraza ambapo kuna Mawakili na vitu kama hivyo. Kama tunataka haki kwa watu wa kawaida, basi ningependa paonekane njia fulani ambazo huyu Wakili anaweza pia akaingilia katika kesi za Mahakama ya Mwanzo ili kuzitoa kwenye dumu hilo lisilokuwa na haki na kulipeleka mahali ambapo angalau mtu anaweza akapata Wakili wa kuweza kumtetea. Bado kuna matatizo makubwa sana kwenye upande huu wa Mahakama ya Mwanzo na Sheria hii nilikuwa ninafikiri ingeweza ikasema kitu fulani ambacho kuna *linking fact* kati ya Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninataka kusema kama tumeamua kwamba haki ni kitu ambacho kimetajwa Kikatiba na ni haki ya kila mtu kuweza kupata utetezi na pia kutoonewa kwa kuwekwa ndani, ningeomba Serikali, ninajua haiwezi ikafanya, lakini ninatoa wito kwa Tume kwa mfano ya Haki za Binadamu, ianze sasa hivi kufundisha watu wa kutoa elimu kwa Watanzania kwamba, ukikamatwa bila sababu, una haki ya kuweza kudai fidia. Mimi ninaona kama jambo hili likichangamkiwa, watu wengi ambao ni waonevu wataona kwamba, kama akimkamata mtu na kumweka ndani bila sababu yoyote, kuna chochote kile ambacho kitaweza kudaiwa. Nimeona kwenye Sheria hii kwamba, kama mtu ataweza kufanya mambo ambayo yataipelekea Serikali, katika *section* ambayo inasema kwamba, kama mtu ataweza kuisababishia Serikali, iko kwenye *amendment*, ikapata hasara kwa sababu ya kuto-*administer justice* sawasawa, basi kuna faini yake ambayo imetengenezwa pale, *I think* ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona tuangalie na upande mwingine, watu wetu wengi wanaamini kabisa kwamba, kukamatwa ni jambo la kawaida, kushtakiwa bila ya sababu ni jambo la kawaida na hakuna utaratibu wowote ambao wao wanaweza kuishtaki Serikali kwa kuwakamata bila ya sababu. Tunahitaji kuwafundisha watu wetu kwamba, wana haki kabisa ya kuipeleka Serikali mahakamani, kwa sababu wamekamatwa bila sababu ya msingi. Ninaona hili ndiyo litaleta suala la haki sawa kwa kila upande.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Asante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA K. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kutoa rambi rambi kwa marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare kuwa Mbunge mpya wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe na Mwanashera Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, kwa hatua nzuri za kuleta muswada huu muhimu sana hasa kwa malengo ya kutenganisha kofia ile ya mashitaka na upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi hasa juu ya mwenendo mzima, mfumo unaotumiwa ule wa kushitaki ambapo chombo hicho hicho hutumika kufanya upelelezi (Polisi). Ni dhahiri kuwa mfumo huu umeonekana kumnyima haki na hasa kwa wanaoshitakiwa mahakamani kuona kutotendewa haki na chombo cha Polisi pale kinapokamata na baadaye kupeleleza.

Kabla ya kuendesha mashitaka mahakamani, mara nyingi tatizo lililolalamikiwa ni pamoja na Kubambikiziwa mashitaka jambo ambalo wao Polisi hutetea mashitaka na kuandaa upelelezi ambao unakandamiza upande ulioshitakiwa, lakini kwa utaratibu huu utaondoa hofu ya kubambikiziwa kesi. Pamoja na nia nzuri ya Wizara bado ninao wasiwasi kuhusu namna Wizara ilivyojiandaa katika kuimarisha utendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (*DPP).* Wasiwasi huu unatokana na ukweli wa ukubwa wa nchi yetu.

Pamoja na musada huu kuainisha kwamba Mkurugenzi atakuwa na wasaidizi na wanasheria, bado haieleweki wasaidizi hawa na wanasheria wataishia ngazi zipi. Upo umuhimu Wakurugenzi Wasaidizi wawepo kila wilaya na maeneo mengine yenye ukubwa (kama mji mdogo) ambapo Mahakama ya Wilaya inafanya kazi. Kufanya hivyo kutaondoa urasimu na hata wingi wa mafaili, kutegemea mtu mmoja ama wale wasaidizi watakaokuwepo Makao Makuu ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa yapo mashitaka mengi sana madogo madogo ambayo uzito wake unaishia Mahakama ya Mwanzo, ni muhimu Muswada ukawa na eneo la kuwa na idara itakayoshughulikia mashtaka peke yake yale ya Mahakama za Mwanzo. Pia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka iongezewe mtu atakayejulikana kama Msajili, jukumu lake kubwa ni kurahisisha na kutenganisha majalada kabla ya kutolewa uamuzi na Mkurugenzi. Aidha, yale yanayostahili kuendelea na mashitaka au yale ambayo hayahitaji kutokuendelezwa kwa mashitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maandalizi mazuri ya kuipa nguvu katika kutenganisha hizi mamlaka, bado Wizara inayo changamoto kubwa kuhakikisha kuwa inajenga mahakama za kutosha, kuongeza idadi ya mahakimu na kuwa na nyenzo bora za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono kuletwa kwa Muswada huu kwa wakati kwa lengo la kutenganisha kazi ya upelelezi na mashtaka.

Aidha, ninasisitiza Kifungu cha 9 (1)(c) na (d) kama kilivyoainishwa kwenye Muswada huu kuwa ni muhimu kuwepo na *control of prosecutions* kwani ni *powers* 20 za *DPP* kwa mujibu wa Katiba, Kifungu 59 B. Katika nchi lazima kuwepo na *Rule of Law*, *Rule of Justice* na kuwepo na *organ* inayowajibika. Hivyo, licha ya kuwa kutakuwepo na *private prosecutors* kama *Income Tax Officers, Labour Officers* na kadhalika ni muhimu *DPP* akawa na *control* ya mashtaka yote ya jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Kifungu cha 27 cha Muswada huu kinaelezea *National Criminal Justice Forum* na kimetoa *Members wa Forum* hii. Ninaafiki *members* wote wa *Forum* na kushauri kuongeza *members* wawili ambao ni *Civilian Personel*, nao wawe mume na mke, wananchi wa kawaida kabisa ili waweze kuona kama *there is Rule of Justice.* Kama ilivyo katika baadhi ya *levels* za mahakama kama *Primary Court* unawakuta *Assessors* (Wazee wa Baraza). Kimsingi Kada hii ni muhimu licha ya kwamba *ignorance of law is not an excuse (*kutokujua sheria si sababu ya kutowajibishwa), lakini Kada hii ni muhimu sana katika *National Criminal Justice Forum.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, ninaomba kuunga mkono hoja na kusisitiza kuwa, sasa Serikali ijiandae na *budget implication* ya kutekeleza Muswada huu haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninatoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, pamoja na kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa kiwango cha juu na mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa uwakilishi wa watu wawili kutoka *Civil Society Organizations* wanaojihusisha na huduma za haki za binadamu, ninaomba kupendekeza pia Wizara kuangalia uwezekano wa kumwongeza Kamishna wa Haki za Binadamu kutoka Tume ya Haki za Binadamu nchini kuingia katika *National Criminal Justice Forum* kwa kuwa ni muhimili mkuu wa haki za binadamu nchini.. Aidha, uwakilishi wa vyombo vya dini nao ni vyema ukafikiriwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wengi hata wale waliokuwa ni Wasemaji Wakuu katika Wizara hii walieleza kwamba, marekebisho haya waliyapata wakati Waziri anasoma. Kwa hiyo, ninapenda kuahirisha kikao mpaka saa kumi na moja ili wale watakaopenda kupitia hii *schedule of amendments* waipitie, kwa

sababu tutakapofika baadaye Naibu Waziri na Waziri watajibu, halafu tutaingia kifungu kwa kifungu. Sasa kwa wale waliosoma na hawakupata mapema basi wahusishe mabadiliko haya na sheria ilivyowasilishwa. Kwa hiyo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.05 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kabla ya kufanya hivyo, niruhusu na mimi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea, nitoe rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Spika, kwako wewe Naibu Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, Wananchi wa Kiteto na ndugu na jamaa wa Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto, ambaye sasa ametutangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kutoa rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mbunge wa Mkuranga, kwa kufiwa na mke wake mpenzi hivi karibuni. Mungu ampe nguvu kwa msiba huo mzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza na kumkaribisha ndani ya nyumba hii Mheshimiwa Mchungaji Getrude Lwakatare ambaye aliapishwa jana asubuhi kuwa Mbunge wa Viti Maalum *CCM.* Nategemea mchango wake mkubwa katika Bunge hili.

Mwisho, ninaomba niwapongeze sana, Wananchi wa Jimbo la Nachingwea, kwa uvumilivu waliouonyesha katika kipindi kigumu cha msimu wa korosho, ambao sasa unamalizika. Matatizo yaliyojitokeza yalikuwa ni ya muda, lakini ninaamini wanaelewa nia njema ya Serikali na niamini kuwa msimu ujao, mambo yatakuwa mazuri kuliko msimu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa niruhusu na mimi nichangie machache juu ya hoja iliyopo mbele yetu. Mchango wangu utajikita katika maeneo ambayo ni ya kiufundi katika hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Pindi Chana, alitoa mchango wake mzuri na tunapenda tumshukuru sana kwa mchango huo. Alitushauri kwamba, katika kile kifungu cha 27, kuongezwe watu wawili ambao siyo wataalam, yaani watu wa kawaida tu wawe katika ile *forum.* Sasa ninafikiri wakati ule naye pia alikuwa hajapata bado ile *Schedule of Amendments.* Katika ile *Schedule of Amendments,* kifungu cha 27(3) kinasema kwamba, *forum* ile inaweza ikateua watu wawili wowote wale ambao inaona itawahitaji kukaa katika *forum* hiyo.

Kwa hiyo, ninafikiri nafasi hiyo ni nzuri, kwa kuteua watu ambao si Wanasheria waingie katika hiyo *forum* na kutoa mchango wao. Alitusihi vilevile tuhakikishe kwamba, tunaweka bajeti ya kutosha ili kuweza kuutekeleza vizuri mradi huu. Mimi ninataka nimhakikishie kwamba, uamuzi huu ni wa Serikali na Serikali inalifahamu hilo. Kwa hiyo, tutaweka bajeti ya kutosha ili tuweze kutekeleza yote yaliyomo katika Muswada huu kwa ukamilifu kabisa.

Mheshimiwa George Simbachawene, naye ninaomba nimshukuru sana kwa mchango wake mzuri. Alichangia vizuri, lakini pia alitaka kujua shughuli ya upelelezi inaishia wapi na shughuli ya kuendesha mashtaka inaanzia wapi. Sasa kimsingi nafasi ya *DPP* katika sheria hii itakuwa ni pamoja na kukagua na kuelekeza upelelezi. Polisi watakamata mtu watampeleleza, kabla hawajatoa ule uamuzi wa kwenda mahali popote, lazima *State Attorney In-charge* au *District State Attorney* atajua kwamba kuna mtu kakamatwa na yeye ataangalia atasema hapa kuna kesi leteni au hapa hakuna kesi mwacheni aende. Kwa hiyo, ule mpango wa kukamata watu na kuwarundika ndani hautakuwepo, utakwisha kabisa. Atawekwa mtu ndani kwa amri ya Mahakama kwamba, umekosa *bail* utakaa ndani, lakini siyo unakamatwa unaweka ndani, halafu upelelezi unaendelea. Jambo hilo tunataka kulikomesha kwa kuanzisha utaratibu huu. Kesi zote zitapelekwa Mahakamani kwa uamuzi wa yule *District State Attorney* pale alipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yule *District State Attorney* na *DDP* mwenyewe, wataelekeza upelelezi kwa maana kwamba, unaweza ukaleta ushahidi, akawaambia hapana hautoshi nendeni mkaangalie *angle* hii na hii. Kwa maana hiyo, ataonekana kama ana-*direct investigation*, lakini hasa atakuwa anatafuta ushahidi ambao anaweza yeye akaenda nao Mahakamani na kuhakikisha kwamba, ile kesi inasimama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wenye uzoefu katika mambo haya kama kule Marekani, kesi hizi zinakaa hata miaka 20. Kuna kesi nilikuwa natazama juzi kwenye *TV*, kesi ya mwaka 1973 *investigation file* bado lipo *open*, kwa sababu ni kesi *complicated* wanatafuta ushahidi, lakini *investigation file* ipo *open*, anayehusika hayupo ndani, lakini *investigation* inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia kumjibu Mheshimiwa John Cheyo pale alipoomba tuweke muda wa kufunga kesi au wa kumweka mtu ndani. Sasa *investigations* zinaweza kukaa *open* kwa muda mrefu, lakini mtu hawezi kukaa ndani bila sababu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kuangalia mchango alioutoa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Ninamshukuru sana ingawa yeye amesema hawezi kuipongeza Serikali, lakini nina hakika, alikuwa anazijua sababu kwa nini Serikali haikuweza kuanzisha mradi huu mwaka 1977, baada ya Tume ya Mheshimiwa Pius Msekwa. Kwa sababu hapo hapo katika mchango wake amesema pia kwamba, Mkoa wa Mwanza ulikuwa na *State Attorneys* watano tu wakati ule. Sasa kwa hali kama hiyo, isingewezekana kuanzisha utaratibu huu. Tulikuwa hatuna watu wa kutosha na sasa

hivi pia tunaanza na mikoa sita tu, kwa sababu mradi huu unahitaji nyenzo nyingi. Kwa hiyo, mikoa sita tunalazimika kuajiri *State Attorneys* 157 zaidi na wafanyakazi wengine wa kawaida karibu 200. Kwa hiyo, si mradi mdogo ni mkubwa, unaotaka *resources* nyingi sana, lakini pia unataka watu wenye ujuzi na uzoefu.

Sasa hivi tunaanza na hii Mikoa sita, tunataka tujifunze matatizo ambayo yanaweza kutokea ili tutakapokwenda nchi nzima tuwe tuna uzoefu na tujue ni kitu gani tunahitaji kufanya ili kuweza kuepukana na matatizo ambayo yanaweza yakaufanya mradi wetu huu usiende vizuri.

Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, alikuwa anazungumzia kuhusu kifungu 10(1)(a), ambacho amesema hakubaliani na maneno "*Defend Criminal Proceedings,"* lakini ukweli ni kwamba ni mara nyingi tu hata katika *Criminal Proceedings*, wakati kesi inatoka katika Mahakama ya Mkoa, kuna suala labda la *bail*, mtu anakata rufaa, Serikali inabidi i-*defend* pale, inakwenda *High Court* ina-*defend* hali kama hiyo. Kwa hiyo, neno hili *Defend Criminal Proceedings* ni sawa, na pia hali hiyo inajitokeza mara nyingi tu. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, akubali neno hili libaki kama lilivyo, kwa sababu ni kweli *State Attorneys* mara nyingi wana-*defend Criminal Proceedings,* wanai-*defend* Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 10(2), Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe alikuwa anasema kwamba, *DDP* anaweza akatumia madaraka yake vibaya kwa sababu ana madaraka makubwa sana ya kwenda kuchukua kesi hata kama kesi hiyo imeanzishwa na mtu binafsi, yaani *Private Prosecution* anaweza bado akaichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitaka niseme kwamba, katika kifungu cha nane cha Sheria hii hii, kinampa misingi *DPP* ya utendaji wa kazi yake na mojawapo ni kuhakikisha kwamba, kuna *public interest* zinalindwa na *interest* za wananchi wote kwa ujumla. Kwa hiyo, atakapokuwa anaichukua kesi namna hii, atakuwa anaichukua kwa kuzingatia utendaji kazi wake, ambao umeelezwa vizuri katika kifungu cha nane na pia katika Katiba yetu na hata katika *CPA*. Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, anajua kwamba *DPP* anahitaji kufanya kazi zake kwa misingi ambayo itahakikisha *public interest* na utendaji wa haki kwa ujumla unazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 27, angekuwa ameangalia katika *Schedule of Amendments*, angekuta wameandika *Director of General Intelligence and Security* na siyo kama walivyoandika katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuungana naye, kuwatetea Wanasheria. Watumishi hawa kweli hali zao hasa kwa mishahara na marupurupu mengine bado hatujafika pale tunapotaka kufikia, lakini tumekuwa tunajitahidi na Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba, tunaboresha hali zao mara kwa mara; tunawapa hiyo *court attire allowance,* tunawapa mpaka *housing allowance* kidogo ili angalau waweze kuishi katika nyumba bora na waweze kuwa nadhifu wanapokwenda kushughulikia shughuli za Serikali. Bado haijafikia tunapopataka, lakini tunafahamu sote kwamba, tuna-*apply*

*policy* ya nchi ambayo tunajaribu kufikia katika kiwango fulani na hii inawahusu wao, pamoja na wafanyakazi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Charles Keenja, kwa mchango wake alioutoa. Yeye amependekeza sheria hii ianze kutumika nchi nzima mara moja na mimi ninakubaliana naye ni jambo nzuri, lakini tulidhani tungeanza kidogo hapa tujenge uzoefu ili tutakapokwenda nchi nzima, tusifanye makosa mengi katika utekelezaji wa Sheria hii. Wazo lake ndiyo hasa nia yetu na sisi twende nchi nzima. Alizungumzia pia kuhusu mazingira ya watumishi na alitaka yaboreshwe ili watumishi wafanye kazi katika mazingira mazuri zaidi na ninakubaliana naye.

Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi, ninapenda naye nimshukuru, amelalamika sana kuhusu hali ilivyo sasa ya Polisi, *VEOs* na *WEOs* kuwa na madaraka makubwa ya kukamata na kutia watu ndani. Kwa uhakika hiyo hasa ndiyo sababu tumeleta Waraka huu ili tuweze kuondoa hayo madaraka huko na kuyapeleka mahali panapohusika. Anayeweza kuweka mtu ndani kwa kipindi kirefu ni Mahakama pekee, wengine wote watamweka mtu ndani wakiwa na sababu, lakini kwa muda wa saa 24 lazima aende Mahakamani kama ana kesi na kama hana kesi tafuta ushahidi, nenda kafanye upelelezi ukipata ushahidi rudi tutakwenda Mahakamani, lakini kwa wakati huu, watu watakaa nje wakati upelelezi unaendelea. Kwa utamaduni huu wa kuweka watu ndani, ndiyo hasa unaopigwa vita na sheria hii na ni imani yetu kubwa kwamba, sheria hii ikipita, basi itatupunguzia sana tatizo hili la mrundikano wa watuhumiwa na mahabusu ambao bado hawajafikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria hii, *DPP* atakuwa na madaraka na uwezo wa kutembelea jela, mahabusu, selo za polisi na sehemu yoyote ile ambapo watu wanawekwa ndani. Atakuwa anakagua pamoja na hali ya haki za binadamu pale, atakuwa anauliza huyu yupo hapa kwa siku ngapi na kwa nini yupo hapa, ameshtakiwa au hajashtakiwa. Kwa hiyo, *DPP* atakuwa na hiyo *supervisory role,* ambayo imo katika sheria hii, atakuwa anakagua, anaangalia, hakuna watu wanaowekwa ndani bila sababu au wanaowekwa ndani kwa kumbabikiziwa kesi kinyume cha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo, alilalamika pia kuwa, kesi zinakuwa ndefu, alitaka kujua kwa muda gani kesi inatakiwa kuendelea; hilo linategemea aina ya kesi, inategemea ukubwa wa kesi, *complexity* zake, kuna kesi nyingine za mauaji, ambazo kutafuta ushahidi siyo rahisi zitachukua muda mrefu, lakini kesi za kawaida tu hizi ambazo ushahidi unaonekana, tunategemea kwa namba ya Mahakimu ambao tunazidi kuwaajiri na utaratibu huu ukiwa *in place,* kesi hazitakaa sana Mahakamani. Kwa sababu mtu akipelekwa ina maana ushahidi upo na ni kuendesha tu kesi, kwa hiyo, hakuna sababu ya kesi kuchukua muda mrefu kama tunavyofanya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mawasilisho yake, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala, alizungumza kuhusu dhana ya uratibu wa upelelezi wa makosa ya jinai, haionyeshi mtenganisho wa kazi ya upelelezi na uendeshaji wa mashtaka na ni kweli kuwa kazi ya msingi ya *DPP* ni kuendesha mashtaka. Hata hivyo, katika ulimwengu wa leo ambapo ni upelelezi unaongozwa na mahitaji ya mashtaka,

yaani *prosecution lead investigation*s ni wazi kwamba, *DPP* ni muhimu kushirikishwa katika hatua zote muhimu baada ya mtu kukamatwa kabla ya kufikishwa Mahakamani ili kuepukana na mtindo wa kumfikisha mtu Mahakamani bila kuwepo na ushahidi wa kukidhi mahitaji ya kesi ya mashtaka. Ndiyo nilikuwa ninasema kwamba, hatapelekwa mtu Mahakamani *unless investigations* zimekamilika, ambazo zitaweza kufanya kesi ikasimame vizuri pale Mahakamani. Kwa kutumia sheria hii inayotarajiwa hasa mafungu ya 18 na 28, yatamwezesha *DPP* na Mheshimiwa Waziri, kutunga kanuni, nyaraka na miongozo itakayowawezesha Watendaji wa Ofisi ya *DPP* na vyombo vya upelelezi, kutekeleza dhana hii kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Watahakikisha kuwa, Polisi na vyombo vya uchunguzi vinapomkamata mtu, aidha vinakuwa na ushahidi wa kuhalalisha kukamatwa kwake na inapobidi kuwekwa mahabusu, saa zilizowekwa na sheria tu ndiyo anakaa mahabusu kabla ya kufikishwa Mahakamani si zaidi ya hapo. *DPP* au Afisa wake, anajulishwa kuwepo kwa mtu anayestahili kufikishwa Mahakamani na kuanzia hapo ndipo ushiriki wa *DPP* unaanzia na kuandaa mashtaka.

*DPP* au mwakilishi wake, kama kuna mambo hayajatimizwa na wachunguzi wale wapelelezi wa kesi, anakaa nao na kutoa maelekezo ya nini kipatikane vinginevyo mtu asifikishwe Mahakamani. Kwa kufanya hivyo, anaratibu nini kipatikane kwa mahitaji ya mashtaka kama tunavyosema hii ni *prosecution lead investigation.*

Fungu la 16(4), linamwezesha *DPP* au mwakilishi wake, kujua taarifa za watu walio mahabusu na atatoa maelekezo. Kwa hiyo, kama kuna watu watawekwa mahabusu kwa kipindi ambacho si sahihi*, DPP* atatoa maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kesi kama za ugaidi, dawa za kulevya, rushwa kubwa, *money laundering* na kadhalika, ambazo mchakato mzima wa upelelezi wake hushirikisha zaidi ya chombo cha upelelezi kimoja, yaani unaweza kukuta *PCCB* wanapeleleza, na Polisi nao wanapeleleza, katika hali kama hii *DPP* atapata fursa ya kuvishirikisha vyombo hivyo kwa pamoja na kuratibu mambo yote ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kesi kama hizi za *money laundering,* unaweza kukuta Polisi wapo, sasa wote hawa wanafanya upelelezi bila kuwa na mtu anayeweza ku-*co-ordinat,e* PCCB pia unaweza kukuta mambo haya hayaendi sawasawa. Kwa hiyo, *DPP* atakuwa na *role* katika kesi za namna hiyo, kuweza kuuratibu upelelezi wa vyombo hivi vinavyohusika. *DPP* peke yake ndiye anaweza kuratibu vyombo hivyo ili kupata kesi yenye sifa kimashtaka. Mafungu 16, 17, 24 na 27, yanaweka mazingira ya kumwezesha *DPP* kufanya kazi kwa pamoja kama timu na vyombo vya upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ya Mwenyekiti pia alizungumzia uteuzi wa hii mikoa sita. Kamati ilishauri Serikali iangalie mambo ya msingi ya kutekeleza katika mikoa sita na wakati huo huo iangalie uwezekano wa kutumia watu au vyombo vingine, wanaoweza kuendeleza kazi hizo hizo katika maeneo yaliyo *key*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa mikoa sita, mahitaji yake yameshaainishwa ndiyo maana Mawakili 157 wameajiriwa na kwa Mikoa iliyobaki fungu 29 linamwezesha *DPP* kuendelea na kazi za udhibiti wa mashtaka kwa kutumia sheria zilizopo. Kwa vile Katiba na Sheria tarajiwa vinamruhusu kutumia aidha, Mawakili waliopo chini yake au Maafisa wengine kutoka vyombo vingine, anaowaona wanazo sifa za kufanya kazi hiyo. Kwa maana labda *tax officers* ambao wanaweza ku-*prosecute*, watu wa *PCCB* ambao wanaweza ku-*prosecute* na wengine kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilizungumzia Wanasheria wa Halmashauri wahusishwe. Katika Muswada huu fungu 22(1), kama ilivyoonekana katika *Schedule of Amendments*, linampa *DPP* uwezo wa kuwateua Wanasheria kutoka kwenye Halmashauri ilimradi ameridhika kuwa wanazo sifa za kuendesha mashtaka na pia mamlaka zao za ajira zimeshirikishwa na kutoa ridhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, wanaweza kuajiriwa *State Attorneys* ambao watakaa katika wizara nyingine au mikoani. Hawa kama *DPP* ataridhika na uwezo wao, anaweza kuwateua kuendesha kesi za Serikali katika sehemu hizo walipo. Kwa hiyo, pamoja na ile mikoa sita, lakini ninafikiri zoezi hili linaweza likaenda katika sehemu nyingine kwa kutumia utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, naye alionyesha wasiwasi ni jinsi gani Wizara ilivyojipanga kusimamia utekelezaji kwa kuzingatia ukubwa wa nchi na haionyeshi hao wasaidizi na Wanasheria wataishia ngazi zipi? Kwa hiyo, upo umuhimu wa Wakurugenzi wasaidizi, kuwepo kwa kila ngazi katika maeneo yenye ukubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya utafiti na kubaini mahitaji halisi yaliyopelekea kuchaguliwa kwa mikoa sita na sasa utekelezaji wake utaanza kwa kuwa Mawakili wamekwishaajiriwa tayari kwa ajili ya mikoa hiyo sita. Wakati utekelezaji wa ajira ya kwanza kwa mpango huu unafanyika mwezi huu, tayari Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara, walishaandikiwa barua na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili watoe msukumo wa upatikanaji wa viwanja kila Mkoa na Wilaya kwa ajili ya kujenga ofisi za mashtaka na palipo na majengo, majengo hayo basi yatolewe kwa Wizara yangu. Utekelezaji umeshaanza na kuna Halmashauri za Wilaya na Miji michache ambazo zimekwishatenga maeneo. Ninazipongeza Halmashauri hizo husika, kwa jinsi zilivyoanza kuitikia katika jambo hili. Tumepata viwanja katika sehemu mbalimbali na wengine wametupa na ofisi ambazo tunaweza tukaanzia kazi katika mikoa hiyo. Sheria tarajiwa, itatoa fursa kwa muundo wa Ofisi ya *DPP* kuongozwa na Wakili wa Serikali wenye uzoefu na muundo utazingatia kuwepo kwa kada nyingine ili kuiimarisha Ofisi ya *DPP*, yaani zile *supporting cadre*. Mungu ya 5 na 7 ya Sheria hii, yanatoa nafasi nzuri ya kuwezesha kuwepo kwa muundo mzuri wa kukidhi mahitaji ya ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie mchango wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambao nilianza kusema kwamba, alikuwa anataka kujua upelelezi na uendeshaji kesi vinatengana wapi. Maelezo kuhusu swali hili kwa kiasi

kikubwa yapo kwenye majibu yangu kwa hoja ya uratibu iliyowasilishwa na Kamati. Hata hivyo, kwa kusisitiza tu ni kwamba, kamwe *DPP* hatafanya upelelezi ila atakachofanya ni kuhakikisha kwamba, vyombo vya upelelezi vinapata mambo muhimu katika kesi ili kujiridhisha kama ni kesi ya kufutwa ama kukiwa na ofisi za upelelezi kwa maana kuwa malalamiko yaliyowasilishwa hayaungwi mkono na ushahidi unaopatikana au mambo ambayo yanafanyiwa kazi ili mtuhumiwa asiachwe huru kwa kuwa eti tu kuna kipengele fulani kinafanyiwa kazi na wapelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumalizia kwa kuliomba Bunge lako Tukufu, liutafakari Muswada huu na kuupitisha ili Sheria hii ipite. Utaratibu huu wa *civilianisation* uanze na tunategemea utafanikiwa, kwa sababu ukianza tutapunguza mambo mengi; mirundikano katika jela na mahubusu itapunguzwa sana. Kesi za kumbabikizwa zitatoweka kabisa, kwa sababu hakuna mtu atakayekuwa na uwezo wa kufanya hivyo, wakati kuna vyombo viwili vimekwishatengana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja hii. Asante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa mara nyingine, ninarudi mbele yako na mbele ya Bunge lako Tukufu, kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini, niliouwasilisha asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukushukuru sana, kwa kuendesha Shughuli za Bunge wakati wakijadili Muswada huu kwa umahiri mkubwa. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wananchi pia, kufuatilia majadiliano juu ya Muswada na hotuba yangu niliyoiwasilisha asubuhi. Muswada huu ni muhimu, kwani nia yake ni kuimarisha na kuboresha utoaji wa haki nchini. Kwa namna ya pekee, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliotoa michango yao ama kwa kauli au kwa maandishi, kwa madhumuni ya kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kama ilivyo utaratibu wetu wa hapa Bungeni, kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, waliochangia humu ndani na hata wakati mwingine. Nianze na waliochangia kwa kuongea nao ni pamoja na Mheshimiwa Mathias Chikawe, ambaye ninyi wenyewe ni mashahidi, mmeona jinsi alivyonisaidia kujibu yale mambo ya kitaalam mkizingatia kwamba, mimi si mtaalam wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ambaye aliwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala asubuhi ya leo, kuboresha Muswada wetu. Ninamshukuru Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Wabunge wengine waliochangia ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo na Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni wafuatao: Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Muswada huu ni kuondoa kero zote zilizotokana na mfumo, ambapo chombo kimoja kilihodhi madaraka yote ya kutuhumu, kukamata, kupeleleza, kufungua na kuendesha mashtaka. Sheria hii sasa itatenganisha shughuli za upelelezi na mashtaka na kwa kufanya hivyo, itaongeza ufanisi kwa sababu Polisi sasa watakuwa na jukumu la kupeleleza na wale Maofisa wa TAKUKURU, Kodi ya Mapato na kadhalika. *DPP* kazi yake itakuwa ni kusimamia na kuendesha mashtaka na atatumia Wanasheria waliobobea na kwa hiyo, katika kutumia utaalam wao na kwa sababu ndiyo kazi yao pekee, napo kutakuwa na ufanisi upande wa kuendesha mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa, Muswada huu utakapopita kuwa sheria, utasaidia sana kupatikana kwa haki na pia kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, sio tu haki itapatikana bali itaonekana kutendeka. Kama nilivyoeleza, utaharakisha maamuzi ya kesi, utapunguza kama si kuondoa kabisa, uwezekano wa kumwonea mtu bila ya sababu, utapunguza muda wa kukaa rumande kama alivyoeleza vizuri sana Mheshimiwa Mathias na hivyo kuondoa tatizo sugu la msongamano katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, jukumu la kuendesha mashtaka ni la kitaalamu. Wanasheria kwa upande wao, wataendesha kesi kwa umakini kwa sababu ni wataalam zaidi wa sheria. Uwezekano wa kesi za kusingizia au kubambikiza hautakuwepo. Mkurugenzi wa Mashtaka, atakuwa anatembelea Magereza na kuona mazingira wanamokuwemo mahabusu na pale ambapo ataona kwamba mahabusu wamewekwa bila sababu na kama itaonekana wamekaa muda mrefu, basi atachukua hatua papo kwa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wametia shaka juu ya mamlaka makubwa ya Mheshimiwa *DPP*. Kama nilivyosema pale mwanzo, kuhodhi madaraka au kuhodhi mamlaka, kunaleta uwezekano wa haki isitendeke, lakini hapa baada ya kutenganisha upelelezi na mashtaka, *DPP* atahusika na mashtaka na wale wengine watahusika na upelelezi. Kwa hiyo, katika kutenganisha hayo mawili, uwezekano wa kutokutoa haki utakuwa haupo, lakini bado Wabunge wamehoji mamlaka ya *DPP*. Mamlaka ya *DPP* yameainishwa katika ibara ya 59(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na inatekelezwa kwa kufuata misingi mitatu ambayo ya kwanza ni nia ya kutenda haki; ya pili ni kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki; na tatu maslahi ya umma na wengi wanauliza maslahi ya umma ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya maneno "*Public interest*" au maslahi ya umma ni kwamba, sheria iweke wazi matumizi ya maslahi ya umma na ibara ya 59(b) na

(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza kwamba, katika kutekeleza mamlaka yake, *DPP* atazingatia maslahi ya umma. Kwa hiyo, hili chimbuko lake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maslahi ya umma katika mantiki hii, inamaanisha manufaa ya Taifa kwa ujumla, ndiyo yaliyo na uzito zaidi ya maslahi ya mtu binafsi. Mazingira dhahiri ya maslahi ya umma yanapopewa uzito zaidi ya maslahi ya mtu binafsi ni wakati panapokuwa na maelewano ya Kitaifa ya kutafuta suluhu juu ya tatizo fulani. Watu wengi na hasa tulipokuwa katika Kamati walisema, kwa mfano, mtu akichukuliwa ardhi yake kwa ajili labda ya kujenga shule au kwa manufaa mengine ya umma, ndiyo basi tukasema ile ardhi inaweza ikachukuliwa kwa ajili ya maslahi ya umma, lakini bado yule mtu atalipwa fidia kama sheria inavyosema.

Kwa hiyo, haya maslahi ya umma hayachukuliwi tu hivyo hivyo kutoa haki ya mtu, lakini ni pale ambapo kama haya maslahi ya umma yatapewa uzito na yeye mwenyewe atanufaika. Kwa mfano, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kurudisha wakimbizi makwao miaka ya 1990, Serikali ilifuta baadhi ya kesi zilizowakabili raia wa Burundi na Rwanda ili taratibu za kuwarudisha makwao zifanyike. Pia kufuatia muafaka uliofikiwa baada ya vurugu za kisiasa za mwaka 2001 Visiwani Zanzibar, kesi za jinai zilizotokana na vurugu hizo zilifutwa na utaona pamoja na kwamba, mtu binafsi amefutiwa lakini maslahi ya umma yamepewa uzito.

Msingi wa maslahi ya umma ambapo *DPP* anatakiwa kuzingatiwa, yana msingi wake katika masharti ya ibara ya 30(1) ya Katiba inayoelekeza kwamba, haki na uhuru wa binadamu ambao misingi yake imeorodheshwa katika Katiba hii, havitatumiwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma. Kwa hiyo, ndugu zangu katika kutumia uwezo wake au mamlaka yake *DPP*, kutokana na kipengele kile cha kati ya maslahi ya umma, si maana yake ni kwamba maslahi haya yanachukuliwa au haki ya mtu inachukuliwa kwa sababu tu *DPP* amependa kufanya hivyo; ni kutokana na hiyo misingi mitatu ambayo nimeeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mathias Chikawe, ameelezea mambo mengi, lakini na mimi ninapenda niseme kwamba, Wapinzani leo asubuhi hawakuunga mkono lakini napo hawakupinga waliwasilisha hoja yao. Ukisoma msitari hadi msitari utaona kwamba, wamekubaliana na Muswada huu na kwamba, umeletwa wakati muafaka. Ninawashukuru sana kwa hilo, mimi ninachukulia kwamba mmeunga mkono Muswada wetu. *(Makofi)*

Vilevile Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe alisema kwamba, haipongezi Serikali, Mheshimiwa Mwakyembe ni Mwanasheria, Wizara ya Katiba na Sheria ni Wizara yake ana maslahi nayo na kutokana na uelewa kama alivyoeleza Mheshimiwa Mathias Chikawe anaelewa ni kwa nini tumechukua muda. Katika kuleta haki nchini au kuona kwamba, haki ionekane inatendeka hili haliwezi kufanyika siku moja ni mchakato unaoendelea. Mambo mengi ambayo yamekuwa kwenye Tume zile mbili za Serikali au tatu yametekelezwa na bado tunaendelea kutekeleza. Utaona kwamba hata uamuzi wenyewe wa kuunda Tume ulikuwa wa Serikali ili kuboresha haki ndani ya nchi yetu.

Kwa hiyo, baada ya Tume kukamilisha kazi bado kulikuwa na umuhimu wa kufanya utafiti kuona sasa ni njia gani au mkakati gani muafaka wa kuchukuliwa ili kuongeza haki kuliko ilivyokuwa kabla ya Tume kuundwa. Kwa hiyo ni mchakato huu ambao umetuleta hapa leo na kutufikisha sisi kuweza kuuleta Muswada huu Bungeni kwa ajili ya ninyi Wabunge kuupitisha. Ninategemea baada ya maelezo yangu na ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe tukitoka hapo nje, atatupa pongezi na ataipa Serikali pongezi kwa kuleta Muswada huu Bungeni.

Kama nilivyosema, nia na dhamira ya Muswada huu ni kuhakikisha kama alivyosema Naibu Waziri kwamba, sasa masuala ya ucheleweshwaji kesi yataboreka, badala yake kutakuwa na kasi na ufanisi. Masuala ya msongamano wa mahabusu kama uhalifu hautaongezeka napo vilevile yataondoka, masuala ya kubambikiza kesi yatakuwa historia ndani ya nchi yetu. Sisi tuweze kufanya yale ambayo tunatakiwa kuyafanya na moja ambalo leo tunapaswa kulifanya ni kupitisha Muswada huu, pamoja na marekebisho yake ambayo kwa kiasi kikubwa, yamezingatia maoni na michango iliyotolewa wakati wa Kamati, nje ya Kamati na ndani ya Bunge leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mambo ambayo Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe aliyasema na ninapenda kumpongeza. Alikumbuka juu ya umuhimu wa kuboresha maslahi ya watumishi au Wanasheria au Mawakili wa Serikali. Mawakili wa Serikali, ninakubaliana kabisa wanastahili kuwa na maslahi bora ili waweze kutenda kazi yao na wakati huo wakiwa *motivated.* Mawakili wa Serikali wanaokoa fedha nyingi za Serikali katika kesi hizi. Nikiangalia uchaguzi wa Tunduru kwa mfano, kulikuwa na mwananchi ambaye alitaka uchaguzi uahirishwe lakini Mawakili wetu wakasimama kidete na kuelezea vizuri Mahakamani, badala ya uchaguzi kuahirishwa ukafanyika kama ulivyopangwa na Serikali au Tume ya Uchaguzi na kwa kufanya hivyo wameokoa fedha nyingi sana.

Vilevile Mawakili hao wanakutana na Mawakili binafsi Mahakamani. Wanajua kwamba, Mawakili binafsi wanalipwa fedha nyingi, lakini wao wanaona heshima kubwa kufanya kazi Serikalini na kuwa Mawakili wa Serikali, hawajali fedha nyingi zinazolipwa kwa wale wenzao. Nikisema hivyo, sisemi kwamba hawastahili kupewa maslahi bora, lakini maslahi bora ya Mawakili yanategemea uwezo wa Serikali yao na kila inapopata nafasi ya kuboresha maslahi ya Mawakili wa Serikali, hatutasita kufanya hivyo. Kila wakati tunajaribu kuihamasisha na kuiomba Serikali ione umuhimu na kuona sababu ya kumwangalia Wakili wa Serikali kama tunavyowaangalia Madaktari au Majaji wenyewe na wale wengine ambao wanafanya kazi za kitaalam. *(Makofi)*

Wakati mwingine ni kweli vilevile kwamba, Mawakili wa Serikali, wanaendesha kesi zinazohatarisha usalama wao kama vile kwa Majaji na Mapolisi. Kwa hiyo, masuala ya maslahi kama ya nyumba na usafiri unaoaminika, Serikali inaifahamu na itafanya kila linalowezekana kila inapopata fedha na pengine kuona basi yale maslahi makubwa sana yanayokwenda kwa Mawakili Binafsi, tunayatafutia njia ya kuweza ku-*share* kati ya hao Mawakili Binafsi na Mawakili wa Serikali. Kwa hiyo, hiyo itakuwa ni njia ya busara

pengine ya kuweza kuona kwamba, tunaangalia namna gani Mawakili wetu wa Serikali wanaweza wakalipwa vizuri ili waweze kutenda kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi sana yamesemwa na michango mingi sana tumeipokea na mizuri sana, majibu mazuri ya kitaalamu yametolewa na Naibu Waziri na mimi mwenyewe hapa nimejitahidi kuyasema hayo kwa upande wa kiraia. Nina hakika Muswada huu ukipita, utakuwa ni kwa maslahi ya Bunge hili, kwa kuona malalamiko ya wananchi wetu na vilevile itaonyesha jinsi Serikali ilivyo sikivu, pamoja na kwamba Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe amesema, imechukua muda mrefu lakini hatimaye Muswada tumeuleta Bungeni. Matumaini yangu ni kwamba, baada ya kuyajibu maoni na michango ya Waheshimiwa Wabunge, sasa tutapitisha Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchini wa Mwaka 2007 *(The National Prosecutions Service Bill, 2007)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 17 pamoja na mabadiliko na mabadiliko (m) na kifungu kidogo cha (5)(b), ambacho kinazungumzia juu ya adhabu ya mtu …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, unazungumzia kwenye mabadiliko ama kwenye *original?*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwenye mabadiliko. Kifungu kile kina mabadiliko *clause* namba 17, halafu unakwenda chini fasili ya tano ambapo kinazungumzia juu ya adhabu.

Ninachotaka kuuliza hapa, hiki kifungu ni kizuri kwa sababu kinazuia mtu kuleta mashtaka ya ovyo ovyo kwa mtu au kumkamata au kumweka ndani. Ninatumaini kwamba, kutakuwa na adhabu hapa. Nilimwuliza Mheshimiwa Waziri, wakati ninachangia; je, kuna utaratibu gani wa kuwaelezea wananchi juu ya uwezo wao na haki yao ya kudai fidia panapokuwa na *wrongful arrest* au kushtakiwa bila sababu yoyote?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa John Cheyo wakati wa majadiliano, aliuliza hivyo na tena namshukuru sana alitoa maoni yake kwamba, tufanye nini Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itoe elimu hiyo. Mimi ninakubaliana naye kwamba, tutatoa elimu hiyo si tu Tume ya

Haki za Binadamu na Utawala Bora na sisi wenyewe tutatoa hiyo elimu, lakini wakati huu huu kwa sababu tuko kwenye Kamati, ingekuwa kwenye Bunge na mimi ningewahamasisha wananchi wajaribu. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge nao wawaeleze wananchi, wajaribu kuzijua hizi sheria, sisi tutatoa nakala nyingi ili wananchi waweze kujua sheria zao lakini ninachukua maoni yake, ninamshukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo umesemaje hapo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Tutawaelimisha wananchi ili wadai fidia kwa mujibu wa sheria, kama watabambikiziwa au watasingiziwa kesi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 31

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchini wa Mwaka 2007 *(The National Prosecutions Service Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa taarifa, ninaomba niutambue mchango mzuri na muhimu wa Mheshimiwa George Simbachawene na mchango wa Mheshimiwa Diana Chilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima, imeufikiria Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka Nchini *(The National Prosecutions Services Act, 2007*) na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu umepita katika hatua zake zote na sasa uko tayari kuwa sheria, pindi Mheshimiwa Rais atakapoweka saini yake. Hatuna majadiliano mengine, isipokuwa *technician,* ninadhani kuna matatizo na *sound system* katika meza hii, imeonekana imekuwa hawasikiki vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, hakuna swali lingine lolote kwa hiyo, ninawashukuru wote waliojadili Muswada huu. Inaonyesha jinsi Wabunge mlivyokuwa, maana mabadiliko yale mengi ni kazi nzuri iliyofanywa na Serikali na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati inayohusika.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.58 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 31 Januari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*